القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

Juzuu - Two (Sayaqulu)

by

Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy

la Mwenyezi Mungu" (kwa nini Utume ukaja upande wetu)? Na hali Yeye ni Mola wetu na Mola wenu? (Mlipokuwa wazuri alikupeni nyinyi. Na mlipoharibika katupa sisi). Na sisi tuna vitendo vyetu, nanyi mna vitendo vyenu; nasi tunajihalisisha kwake tu. (Nyinyi mnaabudu Masanamu)

140. Mnasema (nyinyi Mayahudi na Manasara) kuwa Ibrahimu na Ismaili na Is–haqa na Yaaqubu na kizazi (chake) walikuwa Mayahudi (kama nyinyi) au Wakristo (kama nyinyi)? Sema: "Je, nyinyi mnajua zaidi au Mwenyezi Mungu? Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule afichae ushahidi alio nao utokao kwa Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na hayo mnayoyafanya."

141. Hao ni watu waliokwishapita. (Hapana faida kujitapa kwa ajili yao). Wao watapata waliyoyachuma, na nyinyi mtapata mliyoyachuma, wala hamtaulizwa nyinyi yale waliyokuwa wakifanya wao; (wala wao hawataulizwa walipwe kwa mnayoyafanya nyiye. Kila mtu atalipwa kwa lake).

142. Karibuni wapumbavu miongoni mwa watu watasema: "Nini kilichowageuza kutoka kibla chao walichokuwa wakikielekea?" Sema: (uwaambie) "Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu; humwongoza amtakae katika njia iliyonyoka."

143. Na vivyo hivyo tumekufanyeni umati bora (kama kibla chenu tulivyokifanya bora) ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe shahidi juu yenu. Na hatukukifanya kibla ulichokuwa nacho

وَلَنَآ أَعْمَٰلُنَا وَلَكُمْ أَعْمَٰلُكُمْ
وَنَحْنُ لَهُۥ مُخْلِصُونَ ﴿١٣٩﴾

أَمْ تَقُولُونَ إِنَّ إِبْرَٰهِـۧمَ وَإِسْمَٰعِيلَ وَإِسْحَٰقَ
وَيَعْقُوبَ وَٱلْأَسْبَاطَ كَانُوا۟ هُودًا أَوْ نَصَٰرَىٰ
قُلْ ءَأَنتُمْ أَعْلَمُ أَمِ ٱللَّهُ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن كَتَمَ
شَهَٰدَةً عِندَهُۥ مِنَ ٱللَّهِ وَمَا ٱللَّهُ بِغَٰفِلٍ عَمَّا
تَعْمَلُونَ ﴿١٤٠﴾

تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُم مَّا
كَسَبْتُمْ وَلَا تُسْـَٔلُونَ عَمَّا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿١٤١﴾ ع

سَيَقُولُ ٱلسُّفَهَآءُ مِنَ ٱلنَّاسِ مَا وَلَّىٰهُمْ عَن
قِبْلَتِهِمُ ٱلَّتِى كَانُوا۟ عَلَيْهَا قُل لِّلَّهِ ٱلْمَشْرِقُ وَ
ٱلْمَغْرِبُ يَهْدِى مَن يَشَآءُ إِلَىٰ صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿١٤٢﴾

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَٰكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِّتَكُونُوا۟ شُهَدَآءَ
عَلَى ٱلنَّاسِ وَيَكُونَ ٱلرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيدًا وَمَا

(5000). Wamekuja baada yake chungu ya Mitume, hata anaitwa Baba wa Mitume. Khalafu baada ya Kupita miaka yote hiyo ndio imeambiwa katika Quran na Hadithi za Mtume—kama tulivyobainisha katika maelezo ya Aya ya 4 ya *Suratul Baqarah*—kuwa sasa baada ya Nabii Muhammad hapewi tena mtu mwengine Utume. Watafedheheka tu maisha Makadiyani na watahizika, kwani wanaitafuta wenyewe hizaya. Na haambiwi "Pole" mtu kwa ugonjwa wa kujitakia.

126. Nabii Ibrahimu alipoiombea kheri nchi ya Makka na akawaombea riziki wakazi wake, aliwaombea wale Waislamu tu. Mwenyezi Mungu akamwambia "La, ukubwa wa dini mbali na riziki mbali. Ukubwa wa dini ndio haupati ila mwema. Ama riziki hapa duniani nitampa yo yote yule, akiwa Mwislamu au akiwa si Mwislamu."

133. Mayahudi walimkanusha Mtume alipowaambia kuwa Nabii Yaaqubu aliwausia watoto wake kufuata Uislamu. Basi Mwenyezi Mungu ndiyo anawaambia "Mlikuwapo nyinyi hata mnakanusha?"

136. Aya hii mara nyingi Mtume akiisoma katika rakaa ya mwanzo ya suna ya Al-fajiri(kabliya), na akisoma katika rakaa ya pili aya ya 64 ya Surat aali-Imran.

138. Watoto wa Kikristo hubatizwa (huchovywa ndani ya maji wanayoyaitakidi kuwa matakatifu). Basi hapo huitakidiwa kuwa washapakika Ukristo. Ndio wanaambiwa hapa kuwa dini ya Kiislamu ni dini inayowafiki tabia (Nature) ya binaadamu wote. Basi nawapakike hii rangi aliyowapaka Mwenyewe Mwenyezi Mungu.

139. Mayahudi na Manasara waliwaambia Waislamu kuwa "Uwongo, Muhammad si Mtume, kwani Mitume hutokana na Mayahudi." Basi ndiyo wakaambiwa wawambie kuwa "Kwani Mola si huyo mmoja tu, na sisi sote si watumwa wake? Si yo yote yule atakayekwenda mwendo mzuri atapendwa na apewe fadhila na Mola wake? Sharti awe Yahudi?"

جعلنا القبلة التي كنت عليها إلا لنعلم من
يتبع الرسول ممن ينقلب على عقبيه ، وإن
كانت لكبيرة إلا على الذين هدى الله ، وما كان
الله ليضيع إيمانكم ، إن الله بالناس لرءوف رحيم ﴿١٤٣﴾

(mara ya kwanza kuwa ndiyo kibla chako sasa na mpaka mwisho wa ulimwengu) ila tupate kumjulisha (atambulikane) yule anayemfuata Mtume na yule anayegeuka akarejea nyuma. Na kwa yakini lilikuwa jambo gumu isipokuwa kwa wale aliowaongoza Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hakuwa mwenye kuipoteza imani yenu. Kwani Mwenyezi Mungu kwa watu ni Mpole sana (na) mwenye rehema.

قد نرى تقلب وجهك في السماء ، فلنولينك
قبلة ترضاها ، فول وجهك شطر المسجد الحرام ،
وحيث ما كنتم فولوا وجوهكم شطره ، وإن
الذين أوتوا الكتب ليعلمون أنه الحق من
ربهم ، وما الله بغافل عما يعملون ﴿١٤٤﴾

144. Kwa yakini tukiona unavyogeuzageuza uso wako mbinguni. Basi tutakugeuza kwenye Kibla ukipendacho. Basi geuza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu (Al-Kaaba); na po pote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu uliko (msikiti huo); na hakika wale waliopewa Kitabu wanajua kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wao; na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda.

ولئن أتيت الذين أوتوا الكتب بكل آية
ما تبعوا قبلتك ، وما أنت بتابع قبلتهم ،
وما بعضهم بتابع قبلة بعض ، ولئن اتبعت
أهواءهم من بعد ما جاءك من العلم ،
إنك إذا لمن الظلمين ﴿١٤٥﴾

145. Na hao waliopewa Kitabu, hata ukiwaletea hoja za kila namna, hawatafuata Kibla chako; wala wewe hutafuata kibla chao, wala baadhi yao hawatafuata kibla cha wengineo; na kama ukiyafuata matamanio yao baada ya kukufikia ilimu, utakuwa miongoni mwa madhalimu (wenye kudhulumu nafsi zao).

---

142. Mtume alipokuwako Makka — anaposali peke yake au pamoja na watu wake — alikuwa akiuelekea ukuta wa kusini wa Al-Kaaba, ili awe kaielekea Al-Kaaba — hiyo iliyoko mbele yake hapo — na iwe kaelekea Baytil Makdis (Baytil Muqaddas) iliyoko Falastin. Aliendelea vivi hivi mpaka alipohama Makka kwenda Madina.

Alipofika Madina — ambayo iko katikati baina ya Makka (kwenye Al-Kaaba) na Baina ya Falastin (kwenye Baytil Muqaddas) ilikuwa haimkiniki kuweza kuvielekea vyote vibla viwili (Al-Kaaba na Baytil Muqaddas) wakati mmoja kama alivyokuwa akiweza alipokuwa Makka.

Basi alikielekea kibla cha Baytil Muqaddas, akakipa mgongo kibla cha Al Kaaba. Alidumu juu ya haya kiasi cha mwaka unusu. Kisha akaambiwa akipe mgongo kibla cha Baytil Muqaddas aelekee cha Al-Kaaba.

Basi hapo ndipo walipotokwa na maneno hao Mayahudi kusema, "Ana nini? Mbona kigeugeu"! Na hali ya kuwa wanaona katika Taurati na Injili kuwa Mtume huyo Muhammad ataelekea huko (Beytil Muqaddas) na huko (Al Kaaba). Wakiyajua haya lakini wakitaka kutukana tu na kuwapoteza watu. Basi Mwenyezi Mungu anamfundisha Mtume Wake jawabu ya kuwajibu.

Masjidul-Aqsa ndio huo Msikiti wa Baitil-Maqdas ambao ulitiwa msingi na Nabii Ibrahim kama alivyoutia msingi Msikiti wa MAKKA (Al-Masjidul-Haraam) na akaujenga. Baada ya kupita miaka 40 tangu kuujenga Msikiti wa Makka ndipo alipoutia msingi Msikiti huu wa Baitul-Maqdis kama ilivyo katika Hadithi ya Mtume Sahihi iliyopokewa na Maimamu hawa:- Muslim, An nassai na Ibnu Maajah.

Kisha ukajengwa vizuri kabisa na Nabii Daud na Nabii Suleiman. Na kusali katika Msikiti huu sala moja ni kama kusali sala hiyo mara elfu katika misikiti mengine, isipokuwa Msikiti wa Madina. Na Imam Al-Bazzar amepokea kuwa kama sala khamsumia.

Na Mtume alisema kama ilivyo katika Hadithi Sahihi iliyopokewa na Maimam wote wa Hadithi kuwa:- "Haifungwi safari kuiyendea Misikiti mengine isipokuwa mitatu hii basi — wa Makka wa Madina na huu wa Baitul-Maqdis.

Na Msikiti huu ulifikwa na maafa mengi — ukavunjwa ukatupwa kabisa kisha ukajengwa tena. Na ilipata kupitiwa na miaka mingi na hali ya kuwa ni kiwanja kitupu.

Kisha katika mwaka wa 17 wa Hijra akautengeza Sayyidna 'Umar Bin Khattab. Basi ukadumu katika mikono ya

146. Wale tuliowapa Kitabu wanakijua (kitendo hiki cha kuelekea Al-Kaaba kuwa ni haki) kama wanavyowajua watoto wao; na baadhi katika wao wanaificha (kila) haki, na hali wanajua.

الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَعْرِفُونَهُ كَمَا يَعْرِفُونَ أَبْنَاءَهُمْ
وَإِنَّ فَرِيقًا مِنْهُمْ لَيَكْتُمُونَ الْحَقَّ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿١٤٦﴾

147. (Huku kuelekea Al-Kaaba) ndiyo haki iliyotoka kwa Mola Wako● Basi usiwe miongoni mwa wanaofanya shaka.

الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿١٤٧﴾

148. Na kila uma ulikuwa na kibla walichokielekea. Basi jitahidini kufanya mema. Po pote mtakapokuwa Mwenyezi Mungu atakuleteni nyote pamoja (siku ya Kiyama), kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mweza wa kila kitu.

وَلِكُلٍّ وِجْهَةٌ هُوَ مُوَلِّيهَا فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ
أَيْنَ مَا تَكُونُوا يَأْتِ بِكُمُ اللَّهُ جَمِيعًا إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ
شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٤٨﴾

149. Na po pote wendako geuza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu (wakati wa Sala). Na hiyo ndiyo haki itokayo kwa Mola wako. Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na yale mnayoyatenda.

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ
الْحَرَامِ وَإِنَّهُ لَلْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ وَمَا اللَّهُ بِغَافِلٍ
عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٤٩﴾

150. Na po pote wendako geuza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu. Na po pote mlipo geuzeni nyuso zenu upande uliko (Msikiti huo) ili watu wasiwe na hoja juu yenu, isipokuwa wale waliodhulumu (nafsi zao) miongoni mwao. (Hao watafuta lo lote tu la kukutukanieni). Msiwaogope niogopeni mimi, na nikutimizieni neema zangu na mwongoke.

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ
الْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ
لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَيْكُمْ حُجَّةٌ إِلَّا الَّذِينَ
ظَلَمُوا مِنْهُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِي وَلِأُتِمَّ
نِعْمَتِي عَلَيْكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٥٠﴾

151. Kama tulivyomleta Mtume kwenu anayetokana na nyinyi, anakusomeeni Aya zetu na kukutakaseni na kukufundisheni Kitabu na hikima na kukufundisheni mliyokuwa hamyajui.

كَمَا أَرْسَلْنَا فِيكُمْ رَسُولًا مِنْكُمْ يَتْلُو عَلَيْكُمْ
آيَاتِنَا وَيُزَكِّيكُمْ وَيُعَلِّمُكُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ
وَيُعَلِّمُكُمْ مَا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ ﴿١٥١﴾

152. Basi nikumbukeni (kwa kunishukuru kwa hii neema niliyokuneemesheni ya kukuleteeni

فَاذْكُرُونِي أَذْكُرْكُمْ وَاشْكُرُوا لِي

Waislamu. Na unazidi kuongezwa na kutengenezwa mpaka ukawa ni Msikiti ambao hauna mfano wake ulimwengu mzima katika uzuri na miujiza iliyomo, kama hilo jabali linalojulikana kwa jina la "Assakhratu-Sharifa". Lakini si kweli kuwa linaning'inia katika anga, haliko chini haliko juu; ila ni ajabu kabisa huo insimamo wake. Na ziko athari nyengine tukufu za kuonyesha ukongwe wake na utukufu wake, kama hilo "Qubbatul Miiraj" na inayoitwa "ATHARU QADAMIN NABIY" na mengineyo.

Lakini viliposhtadi vita vya "CRUSADES" (HURUBUSSALIB) — vita vya Msalaba — vita vikubwa kabisa baina ya Waislamu na Wazungu, iliitekwa hii nchi ya Baitul-Maqdis katika mwaka 492 A.H. Na huu Masjidul-Aqsa ukaingia katika mikono ya Wazungu na Misikiti mengine mitukufu, yote iliyokuwa hapo. Ikavunjwa hishima yake kabisa. Ikawa si mahala pa ibada tena ila mahala pa kufugiwa nguruwe na majibwa na mbuzi na kondoo. Mwenyezi Mungu ana subira.

Hata alipotawala Misri Mfalme Mkubwa Salahud-Din Al-Ayyuby – alichuma nguvu kubwa, akaingia kuwatoa Wazungu nchi za Waislamu. Basi katika mwaka 583 A.H. Baitil-Maqdis na Misikiti yake yote ikawa katika Dola ya Kiislamu tena; mpaka 1918 ilipoingia katika mikono ya Kiingereza kwa Himaya tu, na hivi kwenye mwezi wa June, 1967 ilipoingia katika mikono ya Mayahudi kwa kutawaliwa khasa. Lakini kwa upesi hivi Inshallah itatoka irejee kuwa ya Waislamu kama ilivyokuwa.

143. Wameambiwa kuwa "Mwenyezi Mungu hakuwa mwenye kuipoteza imani yenu", ili kuwapa habari kuwa hizo Sala zao walizozisali mwaka unusu kwa kuelekea Baytil Muqaddas hazikupotea bure — watapewa thawabu zake kwani hayo yalikuwa vile vile kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Imebainishwa hapa kuwa uma wetu

Mtume) (Nami) nitakukumbukeni; na nishukuruni wala msinikufuru.

153. Enyi mlioamini! Jisaidieni (katika mambo yenu) kwa subira na Sala; bila ya shaka Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaosubiri.

154. Wala msiwaite wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu wafu, bali wahai (uhai wa Kiakhera, wa Kiroho, hatujui kaifia yake, kama alivyosema), lakini nyinyi hamtambui.

155. Na tutakutieni katika msukosuko wa (baadhi ya mambo haya); hofu na njaa na upungufu wa mali na wa watu na wa matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri

156. Ambao uwapatapo msiba husema: "Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye tutarejea (atatupa jaza yake)"

157. Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na rehema; na ndio wenye kuongoka.

158. Hakika Safaa na Marwa (Majabali Mawili yanayofanyiwa ibada ya Kusai huko Makka) ni katika alama za kuadhimisha dini ya Mwenyezi Mungu. Basi anayehiji kwenye nyumba hiyo au kufanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka (vilima)

وَلَا تَكْفُرُونِ ﴿١٥٢﴾
يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا ٱسْتَعِينُوا بِٱلصَّبْرِ وَٱلصَّلَوٰةِ ۚ
إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿١٥٣﴾
وَلَا تَقُولُوا لِمَن يُقْتَلُ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ أَمْوَٰتٌۢ ۚ
بَلْ أَحْيَآءٌ وَلَٰكِن لَّا تَشْعُرُونَ ﴿١٥٤﴾
وَلَنَبْلُوَنَّكُم بِشَىْءٍ مِّنَ ٱلْخَوْفِ وَٱلْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ
ٱلْأَمْوَٰلِ وَٱلْأَنفُسِ وَٱلثَّمَرَٰتِ ۗ وَبَشِّرِ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿١٥٥﴾
ٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَٰبَتْهُم مُّصِيبَةٌ قَالُوٓا إِنَّا لِلَّهِ
وَإِنَّآ إِلَيْهِ رَٰجِعُونَ ﴿١٥٦﴾
أُولَٰٓئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَٰتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ ۖ
وَأُولَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُهْتَدُونَ ﴿١٥٧﴾
إِنَّ ٱلصَّفَا وَٱلْمَرْوَةَ مِن شَعَآئِرِ ٱللَّهِ ۖ
فَمَنْ حَجَّ ٱلْبَيْتَ أَوِ ٱعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَن يَطَّوَّفَ

---

huu, uma wa Nabii Muhammad s.a.w., ndio bora kuliko uma zote zilizopita, kwa sababu nyingi. Na moja kubwa ya sababu hizo ni kuwa — kama ilivyobainishwa katika Aya ya 110 ya *Surat Aali Imran* — kuwa wanaamrishana mema na kukatazana mabaya. Na sura nyingine nyingi zimeamrisha haya pia. Basi natukamatane sana sana na sifa hii au tutaukosa ukubwa huu, itufike laana iliyowafika uma zilizo-tangulia kwa kuwa hazikuwa zikiamrishana mema wala kukatazana mabaya. Kila mmoja alikuwa anashughulika na yake tu hana haja na mwenzake; kama ilivyobainishwa katika Aya ya 78 na 79 za *Suratul Maaida*.

Kila Muislamu sharti: (1) Ayashughulikie mambo ya wenzake kama anavyoshughulikia yake; (2) Na awapendelee anayojipendelea, na (3) Awafanyie anayopenda wamfanyie 'mambo Kikowa' — Ukifanya utafanyiwa.

Na anayewafanyia wenziwe hayo mema, na yeye afanyiwe ili azidi kuendelea na asije akavunjika moyo akayawachia, akasikitika kama alivyosikitika mtu huyu aliyesema:

| | |
|---|---|
| Nami nalitaahadi | Kichango kuwa ni changu |
| Haona hapana budi | Ni machezo na wenzangu |
| Haya sikuyafanidi | Kukosa hishima yangu. |

Au asije akawavunja watu nyoyo wasifanye mema tena kama aliyewavunja nyoyo huyu aliyesema:-

| | |
|---|---|
| Zema zinapandwa wapi | Hazipalilive |
| Ninunue na madoo | Maji nitiliye |
| Kama zema zinalipwa | Ningelipwa miye |

144. Mtume -- muda wote huo wa mwaka unusu alioelekea Baytil Muqaddas — alikuwa na hamu apewe amri upesi upesi ya kuielekea Al-Kaaba. Ilipoteremka amri ya kuielekea Al Kaaba, Mtume S.A.W. alikuwa yuwasalisha sala ya Adhuhuri. Mtume S.A.W. aligeuza Mihrab (kwa kugeuka upande aliyokuwa ameelekea; akaelekea alikoamrishwa) yeye pamoja na Maswahaba zake bila ya kuivunja sala yao.

145. Yaani Mayahudi hawatafuata kibla cha Manasara wala Manasara hawatafuata kibla cha Mayahudi kwa kuwa wote wakaidi, hakuna anayeikubali haki japo anaitambua. Basi Mwislamu asiwe hivi. Inataka anapoiyakinisha haki aifuate baada ya kuwa na yakini barabara kuwa hiyo ni haki. Kama vile Sheikh Fulani kumwona Sheikh Fulani kasema neno la haki au kajibu vilivyo, basi namfuate na amtie nguvu, siyo apinge kwa kuwa hakusema yeye, ajitahidi kuyatakia upogo japo kuwa hayana upogo. Na vile vile haya madhehebu ya Kiislamu. Ikiwako kauli

بِهِمَا ۚ وَمَن تَطَوَّعَ خَيْرًا فَإِنَّ اللَّهَ شَاكِرٌ عَلِيمٌ ﴿١٥٨﴾

hivyo viwili; na anayefanya wema (atalipwa) kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye shukurani na Mjuzi (wa kila jambo).

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنزَلْنَا مِنَ الْبَيِّنَاتِ وَالْهُدَىٰ مِن بَعْدِ مَا بَيَّنَّاهُ لِلنَّاسِ فِي الْكِتَابِ ۙ أُولَٰئِكَ يَلْعَنُهُمُ اللَّهُ وَيَلْعَنُهُمُ اللَّاعِنُونَ ﴿١٥٩﴾

159. Hakika wale wanaoficha tuliyoyateremsha — nazo ni hoja zetu zilizo wazi na uwongozi, baada ya sisi kuzibainisha kwa watu Kitabuni — hao anawalani Mwenyezi Mungu, na wanawalani (kila) wenye kulani

إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا وَأَصْلَحُوا وَبَيَّنُوا فَأُولَٰئِكَ أَتُوبُ عَلَيْهِمْ ۚ وَأَنَا التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٦٠﴾

160. Ila wale waliotubu na kutengeza na kubainisha (yale waliyokuwa wakiyaficha), basi hao nitawapokea, na mimi ni Mwenye kupokea toba na Mwenye rehema.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارٌ أُولَٰئِكَ عَلَيْهِمْ لَعْنَةُ اللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١٦١﴾

161. Hakika waliokufuru na wakafa hali ni makafiri, hao iko juu yao laana ya Mwenyezi Mungu na ya Malaika na ya watu wote

خَالِدِينَ فِيهَا ۖ لَا يُخَفَّفُ عَنْهُمُ الْعَذَابُ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿١٦٢﴾

162. Humo (kwenye adhabu ya laana — Motoni) watakaa daima. Hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa muda wa kupumzika.

وَإِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ ۖ لَّا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَٰنُ الرَّحِيمُ ﴿١٦٣﴾

163. Na Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Yeye ambaye ni Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo; (zote mneemeshaji ni Yeye).

---

fulani katika madhehebu fulani imemtulilikia zaidi — kwa hoja na dalili — kuliko kauli ya madhehebu yake, anayo haki ya kufuata kauli hiyo kuliko kauli ya madhehebu yake iliyokosa dalili yenye nguvu. Juu yetu kufuata lililo la haki. Haki, haki yake Ifuatwe, siyo Ikumtwe (Ikung'utwe).

Na madhehebu za haki za Kiislamu zinajulikana: na zinazojigamba kuwa za Kiislamu — wala si za Kiislamu — zinajulikana, kama madhehebu ya Makadiyani (Waahmadiya wa Kadiani). Hao hawakubaliwi kuwa Waislamu maadamu wanasema kuwa Ghulam Ahmad wao huyo kuwa mtume. Mtu anayemkubalia Utume mtu mwengine kuwa kapewa Utume baada ya Nabii Muhammad ni kafiri; na huyo anayejidai huo Utume ni kafiri zaidi. Quran yote nzima inasema *Min qablika* yaani Mitume wa haki ni wale Mitume wa kweli waliopewa Utume kabla yako Nabii Muhammad. Hapana katika Quran *Min Baadika* yaani wakapata Utume baada yako.

Na huko kusema kwao 'Kitabu ..... kimesema kuko kupewa Utume baada ya Nabii Muhammad' ni uwongo kabisa au ni maneno ya vitabu visivyokubaliwa, vinavyosema kinyume na inavyosema Quran na Hadithi Sahihi za Mtume. Basi natutahadhari sana sana kukubali kupotezwa na wapotofu hao wapotezaji. Wanataka mpotee kama walivyopotea (wao) kama anayvosema Mwenyezi Mungu katika Aya nyingi za Sura nyingi za Quran, kama Aya ya 89 ya *Suratun Nisaa* na Aya 44 ya hii hii *Suratun Nisaa*.

150. Watu walio waovu kabisa hata ukweli namna gani ukiwadhihirikia hawaukubali. Bali hutafuta vipengeepengee vya kutukania, japo havipo. Basi hao inataka mtu asiwajali.

152. Kushukuru kukubwa kabisa ni kuitumia neema — hiyo uliyopewa — katika mahala pake, kisha ndiyo kusema *Al-Hamdulillah.* Umepata neema kubwa kabisa kupata Uislamu, basi kuwa Muislamu kamili — kwa maneno yako na vitendo vyako na mwendo wako na kila chako. Nje yako na ndani yako iwe sawa.

153. Mtu lazima afikwe na misukosuko kwani ndiyo inayomtengeneza na kumtakasa na kumsafisha, kama inavyotakaswa dhahabu kwa kutiwa kwenye moto, na kutakaswa vingine kwa kukwatuliwa (kukatuliwa), na vingine kwa kunolewa, na vingine kwa kuoshwa, na vingine kwa kusuguliwa na vingine kwa ... Basi astahamili Mwislamu akifikwa na misukosuko; asimame imara, azidi kujitahidi kuendelea mbele; na huku anamwomba Mwenyezi Mungu. Atafanikiwa tu japokuwa baada ya muda mrefu kabisa. Anayejitahidi atapata tu. Mstahamilivu hula mbivu. Pasemwe:–

Mlokisema hayawi Mbona leo yamekuwa

Wala usiseme 'kuna watu wananiroga, wananitendea, wananihusudu ... ndiyo maana hayawi' Yatakuwa tu saa

164. Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na (katika) kuandamizana usiku na mchana, na (katika mwendo wa) vyombo ambavyo hupita katika bahari kwa (kuchukua vitu) viwafaavyo watu, na (katika kumiminika) maji aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mawinguni, na kwa (maji) hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake, na akaeneza humo (ulimwenguni kwa sababu ya maji hayo) kila aina ya wanyama; na katika mabadiliko ya pepo, na mawingu yanayoamrishwa kupita baina ya mbingu na ardhi; bila shaka (katika haya) zimo Ishara kwa watu wenye akili (kuwa yuko Mwenyezi Mungu na ni Mmoja tu).

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمٰوٰتِ وَ الْأَرْضِ وَ اخْتِلَافِ
الَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَالْفُلْكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ
بِمَا يَنْفَعُ النَّاسَ وَمَآ أَنْزَلَ اللّٰهُ مِنَ السَّمَآءِ
مِنْ مَّآءٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ
فِيهَا مِنْ كُلِّ دَآبَّةٍ وَّتَصْرِيفِ الرِّيٰحِ وَ السَّحَابِ
الْمُسَخَّرِ بَيْنَ السَّمَآءِ وَ الْأَرْضِ لَأٰيٰتٍ
لِّقَوْمٍ يَّعْقِلُونَ ﴿١٦٤﴾

165. Na katika watu kuna wanaofanya waungu wasiyekuwa Mwenyezi Mungu. Wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana. Na laiti waliodhulumu nafsi zao wanaijua (balaa itakayowapata) watakapoiona adhabu (siku hiyo ya Kiyama), kwa kuwa nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu (siku hiyo — hakuna masanamu wa kuwashufaia wala mengineyo) na kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَّتَّخِذُ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ أَنْدَادًا
يُّحِبُّوْنَهُمْ كَحُبِّ اللّٰهِ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا أَشَدُّ حُبًّا لِّلّٰهِ
وَلَوْ يَرَى الَّذِيْنَ ظَلَمُوْٓا إِذْ يَرَوْنَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ
لِلّٰهِ جَمِيْعًا وَّأَنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعَذَابِ ﴿١٦٥﴾

---

yake ikifika. Sema kila mara:–

Sitoayisi tamaa
Nangojea yangu saa
Nifurahi na jamaa
Kufanikiwa muradi
Saa ya sada na sudi
Landikwalo halirudi.

Uwasimange kimoyomoyo useme:–

Mlimkisema
Liwe jambo hili
Andikalo Mola
Hebu lifuteni
Na kushiriki
Halifanyiki
Halifutiki
Nasi tuone.

154. Wamepachika katika Aya ya *Al Baqarah* waliyoita ya 25 kuwa uhai wa Akhera ni wa kiroho tu. Tumebainisha katika Aya ya 24 na 25 za hii *Suratul Baqarah*, kwa kila hoja, kuwa maisha ya Akhera ni ya roho na kiwiliwili — tusichezewe na makafiri.

158. Katika Ibada ambazo hazisihi kufanywa ila Makka ni hizi (a) Hija; na (b) Umra. Na takriba zote mbili hizi ni sawa sawa ila zinakhitalifiana kidogo tu.

Moja katika hitilafu yao ni kuwa Hija haifanywi ila katika miezi makhususi: na mwisho wa miezi ya hija ni kumi la mwanzo la Mfungo tatu. Ama Umra hufanywa mwezi wo wote uutakao. Na katika Umra hupunguka jambo moja — huwa hapana kwenda kusimama katika Uwanda wa Arafa.

Ama mengine ni sawa. Nayo ni: (1) Kuzunguka Al-Kaaba mara 7; (2) Kwenda mbio mara 7 baina ya majabali hayo mawili ambalo moja linaitwa Safaa na moja linaitwa Marwa; (3) Kunyoa nywele au kuzikata.

Majabali hayo kabla ya Uislamu yalikuwa yamewekwa juu yake masanamu; na makafiri wakiyaabudu. Basi ulipokuja Uislamu Waislamu wengine waliona labda si vizuri kufanya ibada hapo penye majabali hayo. Basi wakaambiwa kuwa 'Si vibaya' maadam masanamu hayo yamekwishaondoshwa; na wao hawafanyi ibada yao hiyo kwa ajili ya masanamu.

159. Ni wajibu wa kila mwenye kujua haki (a) aikubali na (b) aifuate na (c) aitangaze na (d) aifundishe. Basi mashekhe na walimu, bahati yao nzuri, wamepata kazi nzuri kabisa. Basi nawafurahi kwa kazi hii — wakiifanya bure au kwa pesa. Basi nawaendelee nayo hata kwa taabu kubwa kubwa kabisa. Na hii ndiyo kazi

166. (Wakumbushe wakati) Waliofuatwa watakapowakataa wale waliowafuata, na hali ya kuwa wamekwisha kuiona adhabu, na yatakatika mafungamano yao.

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتُّبِعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا
وَرَأَوُا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ ﴿١٦٦﴾

167. Na watasema wale waliofuata, "Laiti tungeweza kurudi (duniani) tukawakataa kama wanavyotukataa." Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu atakavyowaonyesha vitendo vyao kuwa majuto yao; wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni.

وَقَالَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا لَوْ أَنَّ لَنَا كَرَّةً فَنَتَبَرَّأَ
مِنْهُمْ كَمَا تَبَرَّءُوا مِنَّا ۗ كَذَٰلِكَ يُرِيهِمُ اللَّهُ أَعْمَالَهُمْ
حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ ۖ وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ ﴿١٦٧﴾

168. Enyi watu! Kuleni vilivyomo katika ardhi, halali na vizuri, wala msifuate nyayo za Shetani (yale anayokuamrisheni). Bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ كُلُوا مِمَّا فِي الْأَرْضِ حَلَالًا طَيِّبًا
وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ ۚ
إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿١٦٨﴾

169. Yeye anakuamrisheni (kufanya) mambo mabaya na machafu, na mumsingizie Mwenyezi Mungu msiyoyajua (yakini yake kuwa kweli kasema hayo au hakusema).

إِنَّمَا يَأْمُرُكُمْ بِالسُّوءِ وَالْفَحْشَاءِ وَأَنْ تَقُولُوا
عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿١٦٩﴾

170. Na wanapoambiwa. "Fuateni aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu" husema: "Bali tutafuata yale tuliyowakuta nayo baba zetu." Je, hata kama baba zao walikuwa hawafahamu cho chote wala hawakuongoka (watawafuata tu)?

وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا
بَلْ نَتَّبِعُ مَا أَلْفَيْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا ۗ أَوَلَوْ كَانَ
آبَاؤُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ شَيْئًا وَلَا يَهْتَدُونَ ﴿١٧٠﴾

171. Na mfano wa wale (wanaowalingania) waliokufuru (kwa inadi tu, si ujinga) ni kama mfano wa yule anayemwita asiyesikia ila sauti na kelele tu. (Wao) ni viziwi, mabubu, vipofu, kwa hivyo hawafahamu.

وَمَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا كَمَثَلِ الَّذِي يَنْعِقُ
بِمَا لَا يَسْمَعُ إِلَّا دُعَاءً وَنِدَاءً ۚ صُمٌّ بُكْمٌ عُمْيٌ
فَهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٧١﴾

---

waliokuja nayo Mitume; basi natuifanye; na ruwaza yetu wawe wao (Mitume) na mwendo wao.

Na kuficha kulikokatazwa si kuficha mambo ya dini tu, bali hata mambo ya ujuzi wa kiduniani.

Na walikuwako watu katika Waislamu waliokuwa na ujuzi barabara wa utibabu wa kila namna na wa mambo mengine ya manufaa chungu nzima. Wakakataa kuwafundisha watu kabisa kabisa au wakakataa kuwafundisha watu chungu nzima, wakawafundisha wachache kabisa tu waliowataka; basi wote hao wameondoka hapa ulimwenguni na dhambi chungu nzima. Anayejua la nafuu sharti alijuvye. Hivi ndivyo unavyosema Uislamu.

Wala asiogope kufundisha, kikweli kweli, yaliyo ya dini na yasiyokuwa ya dini, kwa ajili ya kuogopa asije 'Mwanafunzi akamshinda Fundi' na 'Jaha ya Mwalimu Ikavunjika' na 'Riziki yake Ikakatika au Ikapunguka'. Riziki na Jaha na mengineyo yote yako katika mikono ya Mwenyezi Mungu.

Ilimu nyingi kabisa za Kiislamu zimepotea kwa huko kufichwa; ndio maana wafichaji wakastahiki laana kwani wamewakosesha watu nafuu kubwa kabisa.

Lakini hao walioharibu wakitengeneza vizuri kabla ya kufa, *Inshallah* watapata salama kama inavyofahamika katika Aya ya 160.

164. Utazame huu mpango wa maneno haya. Mwenyezi Mungu ni MMOJA tu. Na moja katika mambo yake ya ajabu ni ule mpango usiokuwa na kombo katika uumbaji wake wa namna kwa namna. Mambo haya ya ajabu ni katika yale ya uzuri, nguvu na manufaa kwa binadamu nafsi yake, na ambayo yanawafikiana na akili na busara za binadamu. Tutaanza kwa utukufu wa mbingu na ardhi na yale masafa makubwa ambapo fikira za binadamu zinatembea. Yanaonesha ni mbali walakini ni karibu sana na maisha yake.

Hikima moja kubwa inayoonekana kila siku, ambayo inapatikana kwa maingiliano ya mbingu na ardhi ni mabadiliko ya mchana na usiku. Hili ni jambo la kawaida, juu ya kuwa mabadiliko haya hutafautika kwa mujibu wa Nyakati na mahala pa dunia. Usiku ni wa mapumziko, na Mchana ni wa kazi. Na tunaikadiria hiyo kazi (kama ilivyoelezwa) kuwa: ni meli nzuri zinazosafiri huku na huku baharini, kwa kuleta muungano na biashara baina ya

172. Enyi mlioamini! Kuleni vizuri tulivyokuruzukuni, na Mumshukuru Mwenyezi Mungu, ikiwa mnamwabudu yeye peke yake.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُلُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا
رَزَقْنَاكُمْ وَاشْكُرُوا لِلَّهِ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿١٧٢﴾

173. Yeye amekuharimishieni mzoga tu na damu na nyama ya nguruwe na kilichotajiwa katika kuchinjwa kwake, jina la asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Lakini aliyefikwa na dharura (ya kula vitu hivi) bila kutamani wala kupita kiasi, yeye hana dhambi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

إِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةَ وَالدَّمَ وَلَحْمَ الْخِنزِيرِ
وَمَا أُهِلَّ بِهِ لِغَيْرِ اللَّهِ ۖ فَمَنِ اضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ
وَلَا عَادٍ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ
رَّحِيمٌ ﴿١٧٣﴾

174. Hakika wale wafichao aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu katika kitabu (chake), wakafadhilisha thamani ndogo (ya kilimwengu kuliko kudhihirisha hayo), hao hawali matumboni mwao isipokuwa moto, wala Mwenyezi Mungu hatawasemeza siku ya Kiyama (maneno ya rehema), wala hatawatakasa; nao watapata adhabu iliyo kali.

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنزَلَ اللَّهُ مِنَ الْكِتَابِ وَ
يَشْتَرُونَ بِهِ ثَمَنًا قَلِيلًا ۙ أُولَٰئِكَ مَا يَأْكُلُونَ فِي
بُطُونِهِمْ إِلَّا النَّارَ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
وَلَا يُزَكِّيهِمْ ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٤﴾

175. Hao ndio waliokhiari upotevu kuliko uongofu, na (wakakhiari) adhabu kuliko maghufira. Je! Wana ujasiri gani wa kuvumilia Moto?

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ اشْتَرَوُا الضَّلَالَةَ بِالْهُدَىٰ وَالْعَذَابَ
بِالْمَغْفِرَةِ ۚ فَمَا أَصْبَرَهُمْ عَلَى النَّارِ ﴿١٧٥﴾

176. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ameteremsha Kitabu (chake) kwa haki, (na wao wakakikataa). Na wale waliokhitilafiana katika Kitabu hiki wamo katika upinzani ulio mbali (na haki).

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ نَزَّلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ ۗ وَإِنَّ الَّذِينَ
اخْتَلَفُوا فِي الْكِتَابِ لَفِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ ﴿١٧٦﴾

---

watu. Kwa hiyo manufaa tuyapatayo katika bahari ni sawa na yale tuyapatayo katika bara. Mvua ni matokeo ya maingiliano baina ya bahari, mbingu na ardhi. Mvua inafanya ardhi kuwa rutuba. Hapa inatukumbusha ile tafauti iliyopo baina ya ukosefu wa uhai unaokuwapo wakati wa Chaka na kuhuika wakati wa Mapando. Hapa tunakumbuka kazi ya vipando na tunavyotumia: ng'ombe na vinyama vingine vya namna mbali mbali. Tafsiri ya "wanyama" ni kubwa. Inachanganya wanyama wanaotambaa, vidudu, na kadhalika; wote hawa wamo katika kutimiza uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Haya yanatupelekea katika mambo ya ajabu ya pepo, sehemu ya hewa ambayo sasa binadamu ndio kwanza anaanza kuichungua na kusafiria. Hizi pepo huyasukuma mawingu katika mbingu yafanye kazi yake. Vile vile zipo kazi nyingine zinazofanywa na mawingu kuliko zile za kuleta mvua. Yale mawingu yanapozama, yanaleta mandhari mazuri wakati wa kuchwa jua; vile vile yanapunguza nguvu za mng'aro wa jua katikati ya mchana. Na zaidi ya haya ni kuwa nyakati zote yanaathiri mambo yote katika mbingu. Hapa tena tunarejea juu ya mbingu, kwa kumaliza maelezo yetu na kulinganisha maisha ya binadamu na Amri na Nguvu za Mwenyezi Mungu, ikiwa tunazo busara za kuona.

165. Ilipoambiwa 'Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana' ni kuonyesha kuwa makafiri hao hawana kuthibiti juu ya waola wao hao. Wakati na misukosuko imekuwa mingi hurejea kwa Mwenyezi Mungu. Lakini Waislamu maisha wanamshika Mwenyezi Mungu—hawana leo mungu huyu na kesho mungu yule. Kuna watu wanayashughulikia yasiyokuwa ya Mungu kuliko ya Mungu; kama wale wanayoyashughulikia majengo ya Makaburi, Mazawiya — kwa kuyafanya mazuri na kuyasafisha na . . . kuliko Misikiti na Vyuo. Na wanashughulikia zaidi hayo maziyara na maulidi kuliko kwenda kulingania dini wasiokuwa Waislamu na kuwafunza walio Waislamu lakini hawana ilimu. Hakuna la kushughulikiwa zaidi kuliko kulingania Uislamu na kuufundisha vilivyo.

166. Inaonyesha khasama itakayokuwa baina ya waliopotezwa na baina ya wale waliowapoteza. Waliowapoteza wataruka waseme "Hatukujuweni sisi! Aliyekutumeni nani mtufuate!"

168. Uislamu hautaki kupindukia mipaka katika kujizuilia wala kupindukia mipaka katika kujiachilia. Mtume

177. Sio wema (tu huo peke yake) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi (katika kusali. Yako na mema mengine). Bali wema (hasa) ni (wa wale) wanaomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na wanawapa mali—juu ya kuwa wanayapenda—jamaa na mayatima na maskini na wasafiri (walioharibikiwa) na waombao na katika (kuwakomboa) watumwa, na wakawa wanasimamisha Sala na kutoa Zaka, na watekelezao ahadi zao wanapoahidi, na wavumiliao katika shida na dhara na (katika) wakati wa vita; hao ndio waliosadikisha (Uislamu wao); na hao ndio wamchao Mungu.

لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَ
الْمَغْرِبِ وَلَٰكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَ
الْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ وَآتَى الْمَالَ عَلَىٰ
حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينَ وَابْنَ
السَّبِيلِ وَالسَّائِلِينَ وَفِي الرِّقَابِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ
وَآتَى الزَّكَاةَ وَالْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا
وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ وَحِينَ الْبَأْسِ
أُولَٰئِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿١٧٧﴾

178. Enyi mlioamini! Mmepewa ruhusa kulipa kisasi katika waliouawa — muungwana kwa muungwana, na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke. Na anayesamehewa na ndugu yake aliyeumia) basi ashikwe kulipa kwa wema; na yeye alipe (na kulipishwa) kwa ihsani. Hiyo ni tahafifu itokayo kwa Mola wenu na ni rehema. Na atakayeruka mipaka baada ya haya, basi yeye atapata adhabu iumizayo.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِصَاصُ فِي
الْقَتْلَى الْحُرُّ بِالْحُرِّ وَالْعَبْدُ بِالْعَبْدِ وَالْأُنْثَىٰ
بِالْأُنْثَىٰ فَمَنْ عُفِيَ لَهُ مِنْ أَخِيهِ شَيْءٌ فَاتِّبَاعٌ
بِالْمَعْرُوفِ وَأَدَاءٌ إِلَيْهِ بِإِحْسَانٍ ذَٰلِكَ تَخْفِيفٌ
مِنْ رَبِّكُمْ وَرَحْمَةٌ فَمَنِ اعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَٰلِكَ
فَلَهُ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٨﴾

---

kaja — kama ilivyo katika Aya ya 32 na ya 57 za *Suratul Aaraf* — kutuhalalishia vilivyo vizuri na kutuharimishia vilivyo vibaya. Basi anakataza hapa Mwenyezi Mungu kuviona ni haramu vilivyo halali, kwa kuona kuwa kufanya hivyo ndio kucha Mungu. Kama kuacha kula mapudingpuding haya na kama hivi.

Katika vya kuliwa vilivyoharimishwa katika Quran ni hivi vitakavyotajwa hapa katika Aya ya 173 ya Sura hii na Aya ya 3 ya *Suratul Maida*.

Na katika Hadithi za Mtume vimeharimishwa katika vyakula vya nchi kavu: (a) Wanyama wanavyoshambulia kwa meno yao au kwa kucha zao au kwa vyote viwili (b) Punda wa mji (si punda milia) (c) Kila kinacholewesha (d) Kinachokula zaidi najisi kuliko kula kisichokuwa najisi (e) Kila kinachodhuru (f) Kila kisichokuwa halali yako (g) Vijidudu, kama mjusi, mende, panya.

Na katika wanyama wa baharini: (a) Kila kinacholewesha (b) Kinachodhuru na (c) Kisichokuwa halali yako.

Vyote vilivyosalia ni Halali. Katuumbia makusudi Mwenyezi Mungu tuvitumie kama alivyosema katika Aya ya 20 ya *Suratula Baqarah* na Aya ya 32 ya *Suratul Aaraf* na nyenginezo.

170. Yaani wamepewa akili na viungo vyengine vya kujulia jema na baya; lakini hawavitumii. Wanajifuatia tu waliyowakuta nayo wazee wao—hawatazami kuwa ni mazuri hayo au mabaya. Na hata wakizinduliwa hawakubali kuzinduka.

173. Hapa Mwenyezi Mungu anatupa habari kuwa wanyama wote wanafaa kuliwa ila 4 hawa tu basi. Na hata 4 hawa kama mtu kashikwa na njaa ya kufa atapata ruhusa kuvitumia kwa kiasi cha kuondosha tu hiyo njaa—sio kushiba khasa.

Na 'Kilichotajiwa katika kuchinjwa kwake jina la Asiyekuwa Mwenyezi Mungu' ni kama wanyama wa muhanga wanaochinjwa kwa ajili ya (a) Kupunga pepo (b) Kutia msingi nyumba (c) Kuchimba kisima (d) Kuuzindika mji, na kama hivi miongoni mwa wanyama wanaochinjwa kwa ajili ya Shetani—ati—asiwadhuru.

Na vile vile wanaingia wanyama wanaochinjwa kwa ajili ya mashindano; kama vile chama fulani (au mtu fulani) kimechinja ng'ombe fulani, cha pili kikachinja zaidi kuliko hao, na kama hivi. Basi hao ni najsi—hawaliwi.

Takriban hivi tu basi ndivyo vilivyoharimishwa katika Quran na katika Hadithi za Mtume. Wengine wakiwa wameharimishwa basi wameharimishwa kwa jitihada za wanavyuoni, kama kuliwa popo, kasa, kaa . . . Wanavyuoni wengine wanasema analiwa na wengine wanasema haliwi. Basi tusigombane kwa jambo namna hilo. Ukitaka utafuata wanavyuoni hawa au wanavyuoni hawa.

وَلَكُمْ فِي الْقِصَاصِ حَيَاةٌ يَا أُولِي الْأَلْبَابِ
لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٧٩﴾

179. Mtakuwa nao uhai (mzuri) katika kulipiza kisasi enyi wenye akili, ili msalimike.

كُتِبَ عَلَيْكُمْ إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ إِنْ تَرَكَ
خَيْرًا الْوَصِيَّةُ لِلْوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ
بِالْمَعْرُوفِ ۖ حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِينَ ﴿١٨٠﴾

180. Mnalazimishwa — mmoja wenu anapofikwa na mauti, kama akiacha mali — kufanya wasia kwa wazazi (wake) na jamaa (zake) kwa namna nzuri inayokubaliwa na Sheria. Ni wajibu haya kwa wamchao Mungu.

فَمَنْ بَدَّلَهُ بَعْدَمَا سَمِعَهُ فَإِنَّمَا إِثْمُهُ عَلَى
الَّذِينَ يُبَدِّلُونَهُ ۚ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٨١﴾

181. Na atakayeubadilisha (wasia) baada ya kuusikia, basi dhambi yake ni juu ya wale watakaoubadilisha; hakika Mwenyezi Mungu analisikia (kila linalosemwa), na analijua (kila linalofanywa).

فَمَنْ خَافَ مِنْ مُوصٍ جَنَفًا أَوْ إِثْمًا فَأَصْلَحَ
بَيْنَهُمْ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٨٢﴾

182. Na wenye kuona kwa mwusiaji kuwa kenda upande kwa kukosea, au kupata dhambi (kwa kufanya dhulma kwake makusudi), akasuluhisha baina yao, basi hatakuwa na dhambi (huyo aliyesuluhisha akatengeneza). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe (na) Mwingi wa Kurehemu.

---

174. Vile kusema 'Wakafadhilisha thamani ndogo . . .' muradi ni kuwa wao wanaogopa kudhihirisha yaliyo ndiyo ili wasije wakakosa kile wanachokipata kwa kufanya hayo yasiyokuwa ndiyo. Kama (a) Nyali za Matanga (b) Kutazamia Manazili. Na kama haya.

177. Yaani ingawa Sala ndiyo nguzo kubwa kabisa ya dini lakini haitoshelezi peke yake; inataka zitiiwe (Zifuatwe) na zile amri nyingine pia kama hizi:

1. Kumwamini Mwenyezi Mungu kama unavyosema Uislamu — pasina kukishirikisha cho chote na Yeye katika kukiabudu, na mengineyo, kama vile kuwaomba maiti na mizimu.
2. Kuamini Kiyama kuwa kipo, ukafanya kila amali za kukufaa huko.
3. Kuamini kitabu cha Mwenyezi Mungu — hii Quran — ukajiepusha na kila baya lililotajwa humu na ukafuata kila jema lililobainishwa humo — kwa mwisho wa jitihada yako.
4. Kuamini Mitume ukajitahidi kufuata mwendo wao, khasa huyu Nabii Muhammad kwani yeye — na wao pia — ndizo ruwaza tulizowekewa kufuata.
5. Kutoa Sadaka japo kitu kidogo kuwapa watu hawa — mbali ile Zaka anayotoa anapokuwa tajiri. Hiyo imetajwa mbali — papa hapa — baada ya kutajwa Sala.
6. Kusimamisha Sala — kama inavyosemwa kila wakati — ndiyo nguzo kubwa ya Uislamu baada ya Shahada. Kisha inafuatiwa na saumu (kufunga ramadhan).
7. Kutoa Zaka.
8. Kutekeleza Ahadi. Kila ahadi unayotoa uitekeleze, kama vile unavyoozwa ukatoa ahadi kuwa (a) Mtakaa kwa uzuri au (b) mtaachana kwa uzuri.
9. Kusubiri kwani kama hutasubiri hutaweza kufanikiwa kabisa.

Na miongoni mwa kusubiri ni (1) Kusubiri na kudumu katika kufanya taa ulizoamrishwa. Na kusubiri na kudumu kuacha uliyokatazwa. Na kusubiri juu ya misukosuko na misiba inayokufika, kutokana na Mungu na inayotokana na watu.

Uislamu umekuja umeukuta Utumwa umetapakaa ulimwengu mzima. Kila mwenye nguvu akimwonea mwenziwe na akimfanya mtumwa, akiwa wa kabila yake au si wa kabila yake. Ilikuwa 'Mnyonge Msonge' 'Mwenye nguvu ndiye mwenye haki.'

Ulipokuja Uislamu mara tu uliondosha Utumwa mpya (ulizuiliya watu wapya kufanywa watumwa), hapana kuoneana tena kwa kufanywana watumwa. Na walihimizwa waliokuwa nao hao watumwa waliowamiliki zamani — wawape uhuru ima: (a) Kwa khiari za hao waliowamiliki, kwa kutaraji thawabu kubwa zaidi alizowawekea Mola Kiama; au (b) Kwa lazima; ikitokea bahati ya kufanya mambo kama haya: (1) Kuua japo kwa kutokusudia (2) Kuharibu Hija kwa ajili ya kuingiliana (3) Kuharibu Saumu kwa ajili ya kuingiliana (4) Kugombana na mke, akaapa kuwa hatamwingilia (kwa muda uliyo) zaidi kuliko miezi 4 (5) Kugombana na mke akamwambia anamwona kama mama yake au mwanawe au maharimu yake yo yote yule (6) Kuvunja kiapo (7) Kutaka huyo

183. Enyi mlioamini! Mmelazimishwa kufunga (Saumu) kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُتِبَ عَلَيْكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا
كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٨٣﴾

184. Siku chache tu (kufunga huko). Na atakayekuwa mgonjwa katika nyinyi au katika safari (akafungua baadhi ya siku), basi (atimize) hisabu katika siku nyingine. Na wale wasioweza, watoe fidia kwa kumlisha masikini. Na atakayefanya wema kwa radhi ya nafsi yake, basi ni bora kwake. Na (huku) kufunga ni bora kwenu. Ikiwa mnajua (haya sasa basi fuateni).

أَيَّامًا مَّعْدُودَٰتٍ ۚ فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ
عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۚ وَعَلَى ٱلَّذِينَ
يُطِيقُونَهُۥ فِدْيَةٌ طَعَامُ مِسْكِينٍ ۖ فَمَن تَطَوَّعَ خَيْرًا
فَهُوَ خَيْرٌ لَّهُۥ ۚ وَأَن تَصُومُوا۟ خَيْرٌ لَّكُمْ ۖ إِن كُنتُمْ
تَعْلَمُونَ ﴿١٨٤﴾

185. (Mwezi huo mlioambiwa mfunge) ni Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa katika (mwezi) huo hii Qurani ili iwe uwongozi kwa watu, na hoja zilizo wazi wa uwongozi na upambanuzi (wa baina ya haki na batili). Atakayekuwa katika mji katika huu mwezi (wa Ramadhani) afunge. Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi (atimize) hisabu (ya siku alizowacha kufunga) katika siku nyingine. Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na pia (anakutakieni) mtimize hisabu hiyo, na (anakutakieni) kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongozeni, ili mpate kushukuru.

شَهْرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِىٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلْقُرْءَانُ هُدًى
لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَٰتٍ مِّنَ ٱلْهُدَىٰ وَٱلْفُرْقَانِ ۚ فَمَن
شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ۖ وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ
عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۗ يُرِيدُ ٱللَّهُ بِكُمُ
ٱلْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ ٱلْعُسْرَ وَلِتُكْمِلُوا۟ ٱلْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا۟
ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٨٥﴾

186. Na waja wangu watakapokuuliza hakika yangu, (waambie kuwa) Mimi niko karibu nao. Naitika maombi ya mwombaji anaponiomba. Basi na waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka.

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِى عَنِّى فَإِنِّى قَرِيبٌ ۖ
أُجِيبُ دَعْوَةَ ٱلدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ فَلْيَسْتَجِيبُوا۟ لِى
وَلْيُؤْمِنُوا۟ بِى لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ﴿١٨٦﴾

---

mtumwa ungwana kwa kujinunua. Na kama haya.

Na utumwa uliopita katika nchi hizi kiasi cha miaka 150 sasa ulipitishwa na (a) Wao kwa wao wenyewe wakazi wa pande hizi na (b) Ukapitishwa na Wazungu wote wa Ulaya na Marekani (khasa hao Marekani); na (c) Ukapitishwa na Waislamu waliokhalifu amri za Kiislamu.

Na kwa Propaganda ya Wazungu — katika kutaka kuficha ubaya wao wa kushajiisha utumwa — wamefanya ubaya wa Waislamu wale wachache kuwa wa Waislamu wote, kuwa 'Tusi la Mwarnesi Litukane wake pia'. Wala si haki kufanya hivi. Lakini basi tu — akutukanaye hakuchagulii tusi, hukuvurumizia tu.

178. Huko kusema 'Muungwana kwa muungwana . . .' ni kuonyesha kuwa kila aliyeua aüawe kwa ajili ya yule aliyemwua—asiuawe mtu mwengine.

Zilikuwa kabila nyingi jeuri: Mungwana wa kwao (wanaojiona ni watukufu) akiua mungwana wa kabila nyingine (wanyonge) wanakataa kumtoa mungwana wao aliyeua ili akauawe; wanatoa mtumwa. Na mtumwa wao (hao jeuri) akiuawa na mtumwa wa kabila nyingine basi hawakubali kumwua mtumwa huyo aliyeua mtumwa wao; wanamwua bwana wake au mungwana mwengine yo yote wa kabila ya bwana wa huyo mtumwa. Na vile vile mwanamke wao hafidiwi kwa mwanamke mwenziwe aliyemwua. Wanamwua mwanamume wa kabila hiyo badala ya huyo mwanamke.

Basi hapa Mwenyezi Mungu anaamrisha usawa na insafu: Aliyeua ndiye atakayeuawa, akiwa mungwana au mtumwa, akiwa mwanamume au mwanamke. Hatauliwa mtu mwengine badala yake. Basi hii ndiyo tafsiri ya kipande hiki cha mwanzo.

Na kipande cha pili kinachosema: "Lakini anayesamehewa na ndugu yake . . ." ni cha kutaja pindi (yule) aliyeuawa mtu wake anapomsamehe huyo mwenye kuua na akamtoza fedha badala ya kumwua. Basi ndiyo inaambiwa hapa kuwa ndugu akimsamehe nduguye (na Waislamu wote ni ndugu) kwa kumtoza fedha badala ya kumwua, basi naamdai kwa taratibu, na huyo naalipe kwa wema — asijifanye mkaidi wa kulipa wala kumzungushazungusha kwa 'Leo Kesho' zisizokwisha.

187. Mmehalalishiwa usiku wa Saumu kuingiliana na wake zenu. Wao ni (kama) nguo kwenu (zilizokugandeni mwilini), na nyinyi ni (kama) nguo kwao. Mwenyezi Mungu anajua kwamba mlikuwa mkizihini nafsi zenu. Kwa hivyo amekukubalieni toba yenu na amekusameheni. Basi sasa changanyikeni nao na takeni aliyokuandikieni Mwenyezi Mungu. Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa Alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni Saumu mpaka usiku. Wala msichanganyike nao, na hali mnakaa Itikafu misikitini. Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi msiikaribie. Namna hivi Mwenyezi Mungu anabainisha hoja Zake kwa watu ili wapate kumcha.

أُحِلَّ لَكُمْ لَيْلَةَ الصِّيَامِ الرَّفَثُ إِلَىٰ نِسَائِكُمْ
هُنَّ لِبَاسٌ لَكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَهُنَّ ۗ عَلِمَ اللَّهُ
أَنَّكُمْ كُنْتُمْ تَخْتَانُونَ أَنْفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ
وَعَفَا عَنْكُمْ ۖ فَالْآنَ بَاشِرُوهُنَّ وَابْتَغُوا مَا كَتَبَ اللَّهُ
لَكُمْ ۚ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ
الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ ۖ ثُمَّ
أَتِمُّوا الصِّيَامَ إِلَى اللَّيْلِ ۚ وَلَا تُبَاشِرُوهُنَّ وَأَنْتُمْ
عَاكِفُونَ فِي الْمَسَاجِدِ ۗ تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا
تَقْرَبُوهَا ۗ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ آيَاتِهِ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ
يَتَّقُونَ ﴿١٨٧﴾

188. Wala msiliane mali zenu kwa batili na kuzipeleka kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu kwa dhambi, na hali mnajua.

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ وَتُدْلُوا بِهَا
إِلَى الْحُكَّامِ لِتَأْكُلُوا فَرِيقًا مِنْ أَمْوَالِ النَّاسِ
بِالْإِثْمِ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٨٨﴾

189. Wanakuuliza juu ya miezi. Sema: "Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili (ya mambo) ya watu (mengine) na ya Hija (zao). Wala sio kufanya wema kuingia majumba kwa nyuma. Bali mwema ni yule anayemcha Mwenyezi Mungu. Na ingieni majumba katika milango yake, na Mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufaulu.

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهِلَّةِ ۖ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ
وَالْحَجِّ ۗ وَلَيْسَ الْبِرُّ بِأَنْ تَأْتُوا الْبُيُوتَ مِنْ
ظُهُورِهَا وَلَٰكِنَّ الْبِرَّ مَنِ اتَّقَىٰ ۗ وَأْتُوا الْبُيُوتَ مِنْ
أَبْوَابِهَا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٨٩﴾

---

Na kipande cha tatu kinatutajia hii rehema aliyotupa Mwenyezi Mungu ya kutuwachia wenyewe khiari. Mwenye kuuawa mtu wake — akitaka (a) Ataiambia Serikali imuue huyu aliyemwulia mtu wake au (b) Atamtoza fedha au (c) atamsamehe bure.

Na kipande cha mwisho kinamhadharisha yule anayesamehe kuwa asijidai kumsamehe huku mbele za watu, halafu akamvizia akamwua au akamdhuru kwa siri.

179. Watakuwa wana uhai mzuri kwa sababu kila mtu atakaa kwa adabu yake kwani anajua kuwa akiua atauawa na akidhuru na yeye atafikishiwa madhara. Katika kujikimbizia madhara nafsi yake yanakimbizika hayo madhara kwa watu wengine.

180. Zamani—kabla haukubainishwa mpango wa kurithi—akiachiwa kila mtu aandikie mali yake jamaa zake kwa namna anayoiona mwenyewe. Basi ndiyo anaambiwa ausie kwa namna nzuri inayokubaliwa na Sharia — asifanye dhuluma wala mapendeleo.

181. Wanaonywa mawasii wasibadilishe wasia. Na inatolewa habari ya kuwa huo wasia ukiwa utaharibiwa na hao mawasii, dhambi wanazo hao mawasii waliogeuza. Ama mwenyewe aliyeusia, Mwenyezi Mungu atampa thawabu kamili kwa yale aliyoyafanya—japo hayakutekelezwa kwani huko si kuharibu kwake yeye; ni kuharibu kwa hao mawasii. Na dhambi za mtu mwengine hazimdhuru mtu mwengine.

182. Imetajwa katika Aya iliyotangulia kuwa hapana ruhusa kubadilisha wasia. Basi haya ni wakati wasia huo unapowafiki mwendo unaotaka Uislamu. Ama ikionekana kuwa wasia huo kaufanyia dhulma ndani yake — kama vile madhalimu kuwausia mali watoto wao wanaume tu, wakawaacha wanawake — basi wakiingia watu wakatengeneza baina ya wale wenye kuusiwa — kama vile kuwatia na hao wanawake katika huo wasia japo kwa kitu kidogo kuliko cha hao wanaume — wakati huo watengenezaji hao hawatapata dhambi wala hao waliotengenezewa.

190. Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni, wala msipindukie mipaka (mkawapiga wasiokupigeni). Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi warukao mipaka.

وقاتلوا في سبيل الله الذين يقاتلونكم ولا
تعتدوا إن الله لا يحب المعتدين ﴿١٩٠﴾

191. Na waueni (hao wanaokupigeni bure) po pote muwakutapo, na muwatowe po pote walipokutoweni; kwani kuwaharibu watu na dini yao ni kubaya zaidi kuliko kuua. Wala msipigane nao karibu na Msikiti Mtakatifu (wa Makka) mpaka wakupigeni huko. Wakikupigeni (huko) basi nanyi pia wapigeni. Namna hivi ndivyo yalivyo malipo ya makafiri.

واقتلوهم حيث ثقفتموهم وأخرجوهم من حيث
أخرجوكم والفتنة أشد من القتل ولا
تقاتلوهم عند المسجد الحرام حتى يقاتلوكم فيه
فإن قاتلوكم فاقتلوهم كذلك جزاء الكافرين ﴿١٩١﴾

192. Lakini kama wakikoma, (basi); na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

فإن انتهوا فإن الله غفور رحيم ﴿١٩٢﴾

193. Na piganeni nao mpaka kusiwe na mateso (wao kuwatesa Waislamu bure), na dini iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Na kama wakiacha basi usiweko uadui ila kwa madhalimu.

وقاتلوهم حتى لا تكون فتنة ويكون الدين
لله فإن انتهوا فلا عدوان إلا على الظالمين ﴿١٩٣﴾

194. Mwezi Mtakatifu kwa mwezi mtakatifu. Na vitu vitakatifu vimeekewa kisasi (vikiondolewa hishima yake). Na wanaokushambulieni, nanyi pia washambulieni, kwa kadiri waliyokushambulieni. Na mwogopeni Mwenyezi Mungu (msiongeze kuliko walivyokufanyieni). Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaomwogopa.

الشهر الحرام بالشهر الحرام والحرمات
قصاص فمن اعتدى عليكم فاعتدوا عليه
بمثل ما اعتدى عليكم واتقوا الله
واعلموا أن الله مع المتقين ﴿١٩٤﴾

195. Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo. Na fanyeni wema, hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.

وأنفقوا في سبيل الله ولا تلقوا بأيديكم إلى
التهلكة وأحسنوا إن الله يحب المحسنين ﴿١٩٥﴾

---

183. Na pia tafsiri yake; "ili mpate kusalimika na magonjwa na mabaya . . ." kwani kufunga kidasturi kunaleta siha nzuri kama ilivyokuja katika Hadithi na kama wanavyothibitisha haya hata madaktari wasiokuwa Waislamu.

184. Wasioweza kufunga ni kama: (a) Vizee sana sana — vilivyo kama watoto wadogo — haviwezi kustahmili njaa; (b) Wagonjwa wasioweza kufunga na hawatarajiwi kupona, kama vile wenye ugonjwa wa Cancer au Kifua kikuu kipevu au Blood Pressure au Baulu Sukkar (Diabetes). Basi watu namna hawa hawafungi; na kila siku kila mmoja atajitolea — au atatolewa — kibaba (ratili urobo) cha chakula kinacholiwa sana katika nchi ile. Na aliye masikini asiyemudu kufanya hivi basi; Mwenyezi Mungu atamsamehe kwani 'Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi ila uweza wake'. Ama (1) Mgonjwa wa kutarajiwa kupona; na (2) Mwenye mimba anayeona taabu ya kufunga; na (3) Mwenye kunyonyesha anayetaabika kwa kunyonyesha: Hawatoi fidia; lakini watalipa zile siku walizofungua — wakati utakapoondoka udhuru wao-kama msafiri. Lakini wengine wamesema kuwa mwenye mimba na mnyonyeshaji wanatoa chakula nao. Na kauli hii imesemwa hata na masahaba. Basi inaweza kufuatwa. Na kile kipande kilichosema 'Atakayefanya wema . . .' ni kuonyesha kuwa ukizidisha kuliko kibaba kila siku ni faida kwako mwenyewe — utapata thawabu zaidi. Na kule kusemwa 'Na huku kufunga ni bora kwenu' ni kuonyesha kuwa kufunga si taklifu aliyotukalifisha tu Mwenyezi Mungu isiyokuwa na faida nasi. Bali ni kitu chenye nafuu nasi ya kiwiliwili chetu na menginyo, kabla ya hayo manufaa yake ya Akhera yanayotungojea. Sasa madaktari wa ulimwengu mzima wanaikubali habari hii ya kuwa kufunga kuna nafuu kubwa juu ya kiwiliwili.

Basi hii ni moja katika alama za ukweli wa dini ya Kiislamu. Limesemwa jambo hili kabla ya miaka 1000 ambalo ndio kwanza sasa wasiokuwa Waislamu wamelitambua.

196. Na timizeni Hija na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na kama mkizuiwa, basi (chinjeni) wanyama walio wepesi kupatikana. (Nao ni mbuzi). Wala msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama hao wafike machinjoni mwao. (Napo ni hapo mahala walipozuiliwa). Na atakayekuwa mgonjwa katika nyinyi au ana vya kumwudhi kichwani mwake (akafanya yaliyokatazwa, kama vile kunyoa), basi atoe fidia kwa kufunga au (kwa kutoa) sadaka au kuchinja wanyama. Na mtakapokuwa salama, basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kisha ndio akahiji, basi achinje mnyama

وَأَتِمُّوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلَّهِ ۚ فَإِنْ أُحْصِرْتُمْ فَمَا
اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۖ وَلَا تَحْلِقُوا رُءُوسَكُمْ حَتَّىٰ
يَبْلُغَ الْهَدْيُ مَحِلَّهُ ۚ فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَرِيضًا
أَوْ بِهِ أَذًى مِنْ رَأْسِهِ فَفِدْيَةٌ مِنْ صِيَامٍ أَوْ
صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍ ۚ فَإِذَا أَمِنْتُمْ فَمَنْ تَمَتَّعَ بِالْعُمْرَةِ
إِلَى الْحَجِّ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۚ

---

185. Anataka Mwenyezi Mungu tutimize hisabu hii ya siku 30 au 29 kwa kuwa ile taathira kamili ya kufunga haitimii mpaka ichukue muda wa siku kama hizi.

Na anataka Mwenyezi Mungu tumshukuru kwa ihsani hizi alizotupa — za kutuamrishia kila ya nafuu na kutuharimishia kila ya madhara, alhamdulillah.

186. Siyo wewe tu kumwomba Mwenyezi Mungu 'Nipe hivi na nipe hivi,' na hali ya kuwa wewe huitikii wito wake wa kufanya mema na kuacha mabaya. Itika na wewe wito aliokwitia.

187. Mwanzo ilipoanzishwa fardhi ya Saumu iliharimishwa watu kuingiliana na wake zao usiku mrefu baada ya kuwa wamewahi kulala, japo kidogo. Wakitaka na waingiliane kabla hawajalala. Basi ilikuwa nzito amri hii juu yao; na wengine waliiasi kidogo. Basi ikatolewa ilani kuwa sasa iko ruhusa — kama kula na kunywa — usiku kucha, mpaka alfajiri ndiyo basi.

Na ilivyoambiwa "Takeni aliyokuandikieni Mwenyezi Mungu" ni kuitia nguvu ile ruhusa iliyotolewa ya kuingiliana — usione wewe kuwa bora nisiingiliane maadam zamani ilikatazwa.

Na ilipoambiwa 'Fungeni Saumu mpaka usiku' muradi ni magharibi — jua likishakuchwa tu; ndio usiku wenyewe uliokusudiwa, kama alivyobainisha hivi Mtume; na akahimiza watu wafungue upesi jua tu likishakuchwa; na wakawie kula daku. Ili kufunga kuwe kwepesi, na Uislamu umekuja kwa mambo mepesi kama ilivyobainishwa kule katika Aya ya 184.

Itikafu ni kutia nia mtu kukaa msikitini kutwa nzima au zaidi au kasoro. Na sana Ibada hii hufanywa mwezi wa Ramadhani. Hatoki humo msikitini ila kwa jambo la dharura sana kama kwenda chooni. Basi muda huo wa kuwa yumo katika Itikafu hana ruhusa kuingiliana na mkewe japo katika huo muda wa kwenda chooni.

189. Masahaba waliuliza nini sababu ya kukhitalifu sura ya mwezi — mara mdogo mara mkubwa. Wakajibiwa kwa wepesi tu kuwa 'Ipate kuwa kipimo ili wapate watu kujua kuwa sasa wako katika mwanzo wa mwezi au kati yake au mwisho wake.'

Kisha wakakatazwa ile ada yao ya upuuzi waliyokuwa nayo zama za Ujahili wao. Nayo ni kuwa mtu akiwa yumo katika Hija basi hana ruhusa kuingia ndani ya nyumba—wala kutoka—katika mlango. Sharti waparamie — kwa ngazi au vinginevyo — kwa uwani au kwa mahala pengine au watoboe tundu katika ukuta wa nyumba wapite huko. Na wenyewe wakiona hivyo ndio kucha Mungu.

190. Hii ni moja katika Aya zinazofedhehi uwongo wa wanaosema kuwa Uislamu umesimama kwa Upanga—kwa kuwapiga watu bure ili waingie Uislamu. Huo ni uwongo. Inaonekana hapa kuwa wanapewa ruhusa wapigane na wale wanaowapiga tu, wala hawana ruhusa kupigana na wasiowaanza.

194. Mwezi wa Mfungo Pili na Mfungo Tatu na Mfungo Nne na Mfungo Kumi (Rajab) ni miezi mitukufu. Na hata hao makafiri wa Kiarabu wa hapo zamani wakiihishimu ila kwa nadra tu ndio wakivunja hishima yake. Basi waliivunja hishima yake safari moja wakataka kumpiga Mtume na Masahaba wake. Basi Mtume akaambiwa kuwa wakivunja makafiri hishima ya miezi hii wakawapiga, na wao nawavunje wawapige — wasifunge mikono wakawa wanauawa tu.

195. Kuacha kujiepusha na makatazo ya Mwenyezi Mungu na kuacha kufuata amri Zake — kama hivyo kuacha kusaidia mambo ya vita vya Jihadi—ni kujiangamiza mtu mwenyewe kwani anatafuta ghadhabu za Mwenyezi Mungu.

Katika mwisho wa Aya walioihisabu kuwa ni ya 196 Makadiyani Wamebadili Shariya ya Mungu, wamesema: "Leo hakuna vita vya dini lakini Jihadi ya kalamu na maneno iko." Waliposema Makadiyani "Leo . . ." wanakusudia siku gani na ya mwezi gani na mwaka gani? Wanakusudia 11.3.53 walipotoa tafsiri yao ya uwongo

aliyesahilika. (Naye ni mbuzi). Na asiyepata, afunge siku tatu katika Hija na siku saba mtakaporudi (kwenu); hizi ni kumi kamili. Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawako karibu na Msikiti Mtakatifu wa Makka. Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.

فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَٰثَةِ أَيَّامٍ فِى ٱلْحَجِّ
وَسَبْعَةٍ إِذَا رَجَعْتُمْ ۗ تِلْكَ عَشَرَةٌ كَامِلَةٌ ۗ ذَٰلِكَ
لِمَن لَّمْ يَكُنْ أَهْلُهُۥ حَاضِرِى ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ ۚ
وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ وَٱعْلَمُوٓا۟ أَنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلْعِقَابِ ﴿١٩٦﴾

197. Hija ni miezi maalumu. Na anayekusudia kufanya Hija katika (miezi) hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika hiyo Hija. Na kheri yo yote mnayoifanya, Mwenyezi Mungu huijua. Na chukueni masurufu (ya kutumia njiani, msiombe). Na hakika masurufu bora ni yale yanayomfanya mtu asiombe (kwa kuwa yanamtosha). Na nicheni Mimi, enyi wenye akili.

ٱلْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَٰتٌ ۚ فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلْحَجَّ
فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِى ٱلْحَجِّ ۗ وَمَا
تَفْعَلُوا۟ مِنْ خَيْرٍ يَعْلَمْهُ ٱللَّهُ ۗ وَتَزَوَّدُوا۟ فَإِنَّ
خَيْرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقْوَىٰ ۚ وَٱتَّقُونِ يَٰٓأُو۟لِى ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿١٩٧﴾

198. Si vibaya kwenu kuitafuta fadhila ya Mola wenu (kwa kufanya biashara njiani mnapokwenda kuhiji). Na mtakaporudi kutoka Arafati mtajeni Mwenyezi Mungu penye Mash'aril Haram. Na mkumbukeni kama alivyokuongozeni. Na hakika zamani mlikuwa miongoni mwa waliopotea.

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَن تَبْتَغُوا۟ فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ ۚ
فَإِذَآ أَفَضْتُم مِّنْ عَرَفَٰتٍ فَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ عِندَ
ٱلْمَشْعَرِ ٱلْحَرَامِ ۖ وَٱذْكُرُوهُ كَمَا هَدَىٰكُمْ
وَإِن كُنتُم مِّن قَبْلِهِۦ لَمِنَ ٱلضَّآلِّينَ ﴿١٩٨﴾

---

au lini kabla ya hapo? Kwa siku ngapi na kwa miezi mingapi na miaka mingapi? Wenyewe Makadiyani wamefasiri Aya walioifanya ya 191 kwa kusema: "Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaowapigeni . . ." Na wakaifasiri kama hivi Aya walioifanya ya 192 na Aya walioifanya ya 194 na nyingine nyingi kabisa zenye tamko namna hili. Na wakaifasiri Aya walioifanya ya 195 namna hivi: "Na anayewashambulieni nanyi pia mumshambulie." Na vile vile Aya zenye tamko hili. Nayo ndiyo tafsiri yake iliyo ndiyo, hawana njia ila wafasiri hivi. Lakini walivyokuwa katika Bara Hindi wamo chini ya Utawala wa Kiingereza, wenye dini isiyokuwa ya Kiislamu — na huyo Ghulam wao akawa KIBARAKA mkubwa kabisa wa dola hiyo wakati wa nguvu zake huko Bara Hindi na kila pahali — ndipo alipomsingizia Mungu akaigeuza Quran, akasema "Sasa hapana vita vya Jihadi" hata wakionewa vipi Waislamu na wakapigwa. Wakubali maoneo hayo ya dhila na kuliwa bunga (Kupigwa bure kwa unyonge).

Ukafiri mkubwa huu kugeuza amri za Quran — kwa ajili ya kutaka kuifurahisha dola ya Kiingereza — na kuwalazimishia Waislamu unyonge. Leo wamehizika, juu ya kuwa—tangu wakati huo—wamekufurika. Leo mungu wao na mabwana wao — dola ya Kiingereza — haiko tena! Haitawali huko kwao Bara Hindi wala huku Afrika ya Mashariki na Magharibi walikokimbilia kuja kuwapoteza Waislamu, kama walivyoamrishwa na huyo bwana wao. Wamehizika na kukhasirika duniani na Akhera. Wamekosa kaa na gando. Baada ya miaka 7 tu hivi tangu kutoka tafsiri yao, dola yao waliyokuwa wakiiabudu — kwa chungu ya fedha iliyokuwa ikiwapa na vyeo vikubwa kabisa iliyokuwa ikiwapatia katika dunia yao yote pia — ili waendelee kupoteza na kupotea ikaondoka. Basi baada ya miaka 7 tu dola ya Kiingereza imeondoka kote huko; wamesalia wao wanazubaazubaa, na watu kuwakhadaa!

| | |
|---|---|
| Watangatanga | Na zuo kwapani |
| Wazengea mema | Hawaoni. |

Mwenyezi Mungu amelitaja katika Quran tamko la *"Qaatiluuhum"* (wapigeni — piganeni nao — mara 12): Katika *Al Baqarah* mara tatu; *Aali Imran* mara moja; *An Nisaa* mara moja; *Al Anfal* mara moja; *At Tawba* mara tano; na katika *al Hujurat* mara moja.

Na watuonyeshe — Makadiyani — mahala pamoja tu katika Quran panaposema "Sasa basi msiwapige — msipigane nao — japokuwa wanakupigeni (wanapigana na nyinyi)."

Na amelitumia Mwenyezi Mungu katika Quran tamko la *"Waqtuluuhum"* (wauweni) mara 5, kama hivi:- Katika *Al Baqarah* mara mbili; *An Nisaa* mara mbili; *At Tawba* mara moja. Nawatuonyeshe wao Makadiyani

199. Kisha miminikeni kutoka mahali wamiminikapo watu wote, (napo ni Arafa), na ombeni samahani kwa Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

ثُمَّ أَفِيضُوا مِنْ حَيْثُ أَفَاضَ النَّاسُ وَاسْتَغْفِرُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٩٩﴾

200. Na mwishapo kuzitimiliza ibada zenu (za Hija), basi mtajeni Mwenyezi Mungu kama mlivyokuwa mkiwataja wazee wenu; bali mtajeni zaidi (Mwenyezi Mungu). Na kuna baadhi ya watu wanaosema: 'Mola wetu! Tupe katika dunia'; nao katika Akhera hawana sehemu (yo yote wala hawajali).

فَإِذَا قَضَيْتُمْ مَنَاسِكَكُمْ فَاذْكُرُوا اللَّهَ كَذِكْرِكُمْ آبَاءَكُمْ أَوْ أَشَدَّ ذِكْرًا ۗ فَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلَاقٍ ﴿٢٠٠﴾

201. Na miongoni mwao wako wasemao: "Mola wetu! Tupe mema duniani na (tupe) mema Akhera, na utulinde na adhabu ya Moto."

وَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿٢٠١﴾

202. Hao ndio watakaopata sehemu yao kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.

أُولَٰئِكَ لَهُمْ نَصِيبٌ مِمَّا كَسَبُوا ۚ وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٢٠٢﴾

203. Na mtajeni Mwenyezi Mungu katika zile siku zinazohisabiwa. Lakini afanyaye haraka katika siku mbili (akarejea) basi si dhambi juu yake; na mwenye kukawia pia si dhambi juu yake, kwa mwenye kumcha Mungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba nyinyi mtakusanywa Kwake.

وَاذْكُرُوا اللَّهَ فِي أَيَّامٍ مَعْدُودَاتٍ ۚ فَمَنْ تَعَجَّلَ فِي يَوْمَيْنِ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ وَمَنْ تَأَخَّرَ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ ۚ لِمَنِ اتَّقَىٰ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٢٠٣﴾

204. Na katika watu kuna ambao kauli zao zinakufurahisha hapa duniani. (Lakini Akhera utabainika uovu wao). Nao humshuhudisha Mwenyezi Mungu kwa yaliyomo nyoyoni mwao, na hali wao wagomvi wakubwa kabisa.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يُعْجِبُكَ قَوْلُهُ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيُشْهِدُ اللَّهَ عَلَىٰ مَا فِي قَلْبِهِ وَهُوَ أَلَدُّ الْخِصَامِ ﴿٢٠٤﴾

---

mahala pamoja tu katika Quran panaposema kuwa "Sasa msiwaue japokuwa wanakuuweni". Hawatapapata maisha yao; na juu ya hivi wanaigeuza Sharia ya Mwenyezi Mungu kama kwamba ni yao au ya Ghulam Ahmad wao.

Na amesema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 194 ya *Suratul Baqarah "Faataduu . . ."* (washambulieni kama walivyokushambulieni). Nawatuonyeshe Aya moja tu katika Quran inayosema "Msiwashambulie hata wakikushambulieni." Na juu ya hivi wanathubutu kuwapoteza Waislamu wakasema: "Leo hakuna vita vya dini, lakini Jihadi ya kalamu na maneno iko". Ama wapotezaji wa dini kweli kweli hawa!

Na akasema Mwenyezi Mungu katika Quran mara 2 *"Walamanintasara wantasaruu . . ."* (wenye kujipigania wanapopigwa hawana lawama). Katika *Suratush Shuaraa* mara moja na katika *Suratish Shuuraa* mara moja. Nawatuonyeshe mahala pamoja tu panaposema "Wanaojipigania wamo katika lawama."

Na akasema mara 5 *Falaa Tahinuu* (msikubali kudhalilika) katika *Aali Imran* mara mbili; *An Nisaa* mara moja; *Muhammad* mara moja. Nawatuonyeshe wao mahala pamoja tu katika Quran paliposema *"Kubalini dhila."*

Na akasema Mwenyezi Mungu mara 2 katika Quran *"Waantumul Aalawna"* (Muwe juu), katika *Surat Aali Imran* na *Surat Muhammad.* Nawatuonyeshe mahala pamoja tu panaposema "Kuweni chini — kubalini udhalilifu". Watahizika maisha Makadiyani hizaya ya bibo (kanju) — kichwa chini, miguu juu!

196. Tumekwishataja nini Hija na Umra katika maelezo ya Aya ya 158.

Ilipoambiwa: 'Na kama mkizuiliwa' ni kuonyesha kuwa ikitokea kutoka msafara wa Hija kwenda Makka ukazuiliwa njiani na Maadui. Basi hawatalazimishwa katika Sharia kudumu na mavazi yao na hukumu zao za Hija au Umra. Bali huambiwa wachinje wanyama hapo mahala walipozuiliwa — watoe nyama sadaka. Na wao

205. Na wanapoondoka, wanakwenda huku na huku katika ardhi kufanya uharibifu humo na kuangamiza mimea na roho. Na Mwenyezi Mungu hapendi uharibifu.

وَإِذَا تَوَلَّىٰ سَعَىٰ فِي الْأَرْضِ لِيُفْسِدَ فِيهَا وَيُهْلِكَ الْحَرْثَ وَالنَّسْلَ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الْفَسَادَ ﴿٢٠٥﴾

206. Na wanapoambiwa, "Mcheni Mwenyezi Mungu," mori wao huwapeleka zaidi kwenda kufanya madhambi hayo. Basi Jahannam inawatosha (kuwatia adabu). Napo ni mahali pabaya kabisa pa kutengenezewa kiumbe (kufikia, kama walivyotengenezewa waovu hawa).

وَإِذَا قِيلَ لَهُ اتَّقِ اللَّهَ أَخَذَتْهُ الْعِزَّةُ بِالْإِثْمِ ۚ فَحَسْبُهُ جَهَنَّمُ ۚ وَلَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿٢٠٦﴾

207. Na kuna katika watu, wauzao nafsi zao kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni mpole kwa watumwa wake.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَشْرِي نَفْسَهُ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ رَءُوفٌ بِالْعِبَادِ ﴿٢٠٧﴾

208. Enyi mlioamini! Ingieni katika hukumu za Uislamu zote, wala msifuate nyayo za Shetani; kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا ادْخُلُوا فِي السِّلْمِ كَافَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ ۚ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٢٠٨﴾

209. Na kama mkiteleza baada ya kukufikieni hoja (za Mwenyezi Mungu) zilizo waziwazi, basi jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.

فَإِنْ زَلَلْتُمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْكُمُ الْبَيِّنَاتُ فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٠٩﴾

210. Kuna jengine wanalongojea ila kuwafikia (adhabu ya) Mwenyezi Mungu katika vivuli vya mawingu, na (kuwafikia) Malaika; na lishe (mara moja) hilo jambo (la kuadhibiwa kwao)? Na mambo yote hurudishwa kwa Mwenyezi Mungu.

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَهُمُ اللَّهُ فِي ظُلَلٍ مِنَ الْغَمَامِ وَالْمَلَائِكَةُ وَقُضِيَ الْأَمْرُ ۚ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٢١٠﴾

211. Waulize kizazi cha Israili, hoja ngapi zilizo wazi tulizowapa? Na anayezibadili neema za Mungu baada ya kumfikia, (Mungu atamuadhibu). Hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.

سَلْ بَنِي إِسْرَائِيلَ كَمْ آتَيْنَاهُمْ مِنْ آيَةٍ بَيِّنَةٍ ۗ وَمَنْ يُبَدِّلْ نِعْمَةَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٢١١﴾

212. Wamependeshwa makafiri maisha ya duniani; na wanawafanyia maskhara Waislamu. Na wale wamchao Mungu watakuwa juu yao siku ya Kiyama. Na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila hisabu.

زُيِّنَ لِلَّذِينَ كَفَرُوا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَيَسْخَرُونَ مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا ۘ وَالَّذِينَ اتَّقَوْا فَوْقَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ وَاللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٢١٢﴾

213. Watu wote walikuwa wa dini moja (ya haki aliyokujanayo nabii Adam) (kisha wakakhitalifiana). Basi Mwenyezi Mungu akawaleta Manabii watoao habari njema na waonyao. Na pamoja nao akawateremshia Vitabu vilivyoshikamana na haki ili

كَانَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً فَبَعَثَ اللَّهُ النَّبِيِّينَ مُبَشِّرِينَ وَمُنْذِرِينَ وَأَنْزَلَ مَعَهُمُ الْكِتَابَ

---

wafungue Hija zao, wapata ruhusa kufanya yale wanayokatazwa katika Hija au Umra kuyafanya; kama kunyoa, kukata makucha, kuvaa nguo zilizoshonwa, kuoa na kama haya.

Na iliposemwa 'Atakayekuwa mgonjwa . . ." ni kuonyesha kuwa mwenye kuhiji ikimlazimikia kunyoa—nayo ni haramu kwake—atanyoa, na kafara yake itakuwa ima (a) Kuchinja mbuzi atoe sadaka nyama yake au (b) Kuwapa chakula masikini sita—kila masikini vibaba viwili au (c) Kufunga siku 3.

Na iliposemwa 'Mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra . . . ni kama tulivyosema katika maelezo ya Aya

vihukumu baina ya watu katika yale waliyokhitalifiana. Na hawakukhitalifiana katika hayo ila wale waliopewa vitabu hivyo; baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi, kwa sababu ya uhasidi (uliokuwa) baina yao. Ndipo Mwenyezi Mungu akawaongoza walioamini kwendea haki katika yale waliyokhitalifiana, kwa idhini Yake. Na Mwenyezi Mungu humwongoza amtakaye kwendea njia iliyonyooka.

بِالْحَقِّ لِيَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ فِيمَا اخْتَلَفُوا فِيهِ
وَمَا اخْتَلَفَ فِيهِ إِلَّا الَّذِينَ أُوتُوهُ مِنْ بَعْدِ
مَا جَاءَتْهُمُ الْبَيِّنَاتُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ ۖ فَهَدَى اللَّهُ
الَّذِينَ آمَنُوا لِمَا اخْتَلَفُوا فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِهِ ۗ
وَاللَّهُ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٢١٣﴾

214. Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, na hali hamjajiwa na mfano wa (yale yaliyowajia) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata Mitume na walioamini pamoja nao wakasema: "Nusura ya Mwenyezi Mungu itafika lini?" Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu.

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ
الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ ۖ مَسَّتْهُمُ الْبَأْسَاءُ وَ
الضَّرَّاءُ وَزُلْزِلُوا حَتَّىٰ يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ
آمَنُوا مَعَهُ مَتَىٰ نَصْرُ اللَّهِ ۗ أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ
قَرِيبٌ ﴿٢١٤﴾

215. Wanakuuliza watoe nini? Sema: "Mali yo yote mtakayoyatoa (yatoeni) muwape wazazi na akraba na mayatima na masikini na wasafiri (walioharibikiwa, na waliokuwa kama hawa). Na wema wo wote mnaoufanya Mwenyezi Mungu anaujua."

يَسْأَلُونَكَ مَاذَا يُنْفِقُونَ ۖ قُلْ مَا أَنْفَقْتُمْ مِنْ خَيْرٍ
فَلِلْوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينِ وَابْنِ
السَّبِيلِ ۗ وَمَا تَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٢١٥﴾

216. Mmelazimishwa kupigana vita (kwa ajili ya dini). Nalo ni jambo zito kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu, nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayejua, (lakini) nyinyi hamjui.

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهٌ لَكُمْ ۖ وَعَسَىٰ أَنْ
تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ ۖ وَعَسَىٰ أَنْ تُحِبُّوا
شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ
لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

217. Wanakuuliza (hukumu ya) kupigana vita katika miezi mitakatifu. Sema: "Kupigana vita katika (miezi) hiyo ni dhambi kubwa. Na kuzuilia watu na dini ya Mwenyezi Mungu, na kumkanusha (Mwenyezi Mungu), na (kuwazuilia watu) Msikiti huo mtakatifu, na kuwatoa humo watu waliomo, ni (dhambi) kubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na kuwazuilia watu na dini yao ni mabaya zaidi

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الشَّهْرِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ ۖ قُلْ
قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ ۖ وَصَدٌّ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ
وَكُفْرٌ بِهِ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِخْرَاجُ أَهْلِهِ مِنْهُ
أَكْبَرُ عِنْدَ اللَّهِ ۚ وَالْفِتْنَةُ أَكْبَرُ مِنَ الْقَتْلِ ۗ

---

158 ya kuwa wenye kwenda Makka hufanya Umra na hufanya Hija — hutanguliza waitakayo. Lakini anayefanya Umra hustarehe kwani siku ile ile anayofika Makka huweza kumaliza amali za Umra zote akawa kama dasturi ya mtu asiyekuwamo katika amali hizo—anafanya kila alitakalo. Mpaka mwezi 8 Mfungo Tatu ndipo anaponuwia Hija, akaingia katika hizo amali za hija ambazo zitamalizika siku ya Sikukuu. Itakuwa ile Hija imemdumia muda wa siku 3 tu hivi. Basi huyo anapata takhfifu kubwa.

Lakini anayeanza Hija mbele anapata mashaka, kwani tangu anapofika Makka anadumu na Hija yake, haiwezi kwisha mpaka siku ya Sikukuu. Pengine inachukua mwezi au zaidi. Khalafu akisha hii Hija anaanza Umra.

Basi yule mwenye kuanza Umra huambiwa (a) Achinje mnyama atoe sadaka nyama yake au (b) Afunge siku 10. Tatu kule kule Makka na saba anaporejea kwao.

Na haya yanawathubutukia watu wasiokuwa wa Makka. Ndipo iliposemwa: "Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake . . ."

197. Miezi ya kusihi kunuwia kuhiji ni mitatu — Mfunguo Mosi, Mfunguo Pili na kumi la mwanzo la Mfunguo Tatu. Haisihi kufanya Hija ila katika miezi hii.

kuliko kuuwa." Wala hawataacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika dini yenu, kama wakiweza. Na watakaotoka katika dini yao katika nyinyi, kisha wakafa hali yakuwa makafiri, basi hao ndio ambao amali zao zimeharibika katika dunia na Akhera. Nao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele.

وَلَا يَزَالُونَ يُقَاتِلُونَكُمْ حَتَّىٰ يَرُدُّوكُمْ عَنْ دِينِكُمْ إِنِ اسْتَطَاعُوا ۚ وَمَنْ يَرْتَدِدْ مِنْكُمْ عَنْ دِينِهِ فَيَمُتْ وَهُوَ كَافِرٌ فَأُولَٰئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۖ وَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢١٧﴾

**218.** Hakika wale walioamini na wale waliohajiri (wakahama kuja Madina) na wakapigania njia ya Mwenyezi Mungu, hao ndio wanaotumai rehema ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أُولَٰئِكَ يَرْجُونَ رَحْمَتَ اللَّهِ ۚ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢١٨﴾

**219.** Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: "Katika hivyo mna madhara makuu na (baadhi ya) manufaa kwa (baadhi ya) watu. Lakini madhara yake ni makubwa zaidi kuliko manufaa yake." Na wanakuuliza watoe nini? Sema: "Vilivyokuzidieni". Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya (zake) mpate kufikiri

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ ۖ قُلْ فِيهِمَا إِثْمٌ كَبِيرٌ وَمَنَافِعُ لِلنَّاسِ وَإِثْمُهُمَا أَكْبَرُ مِنْ نَفْعِهِمَا ۗ وَيَسْأَلُونَكَ مَاذَا يُنْفِقُونَ قُلِ الْعَفْوَ ۗ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١٩﴾

**220.** (Mfikiri) katika (mambo ya) dunia na (mambo ya) Akhera. Na wanakuuliza juu ya mayatima. Sema: "Kuwatendea mema ndivyo vizuri. Na kama mkichanganyika nao (ndivyo vyema vile vile), kwani ni ndugu zenu; na Mwenyezi Mungu anamjua fisadi na mtenda mema. Na angalipenda Mwenyezi Mungu angalikutieni katika udhia. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima."

فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۗ وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الْيَتَامَىٰ ۖ قُلْ إِصْلَاحٌ لَهُمْ خَيْرٌ ۖ وَإِنْ تُخَالِطُوهُمْ فَإِخْوَانُكُمْ ۚ وَاللَّهُ يَعْلَمُ الْمُفْسِدَ مِنَ الْمُصْلِحِ ۚ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَأَعْنَتَكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٠﴾

**221.** Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini. Na mjakazi mwenye kuamini ni bora kuliko muungwana mshirikina, hata ingawa akupendezeni. Wala msiwaoze wanaume washirikina

وَلَا تَنْكِحُوا الْمُشْرِكَاتِ حَتَّىٰ يُؤْمِنَّ ۚ وَلَأَمَةٌ مُؤْمِنَةٌ خَيْرٌ مِنْ مُشْرِكَةٍ وَلَوْ أَعْجَبَتْكُمْ ۗ وَلَا تُنْكِحُوا

---

Tena imehimizwa mtu awe mwema kweli kweli siku zote hizo atakazokuwamo katika Hija.

Na ilivyoambiwa 'Chukueni masurufu' ni kuwakataza watu wasende kuhiji na hali ya kuwa hali zao si nzuri, wanapita wakiomba watu. Sio mwendo wa dini huo.

**198.** Wanaokwenda kuhiji wanaweza kuchukua biashara zao wakiuza njiani na wanaweza kufanya biashara huko Makka, haikatazwi. Uislamu unashughulikia yote mawili—dunia na Akhera.

*Mash'aril Haraam* ni mahali huko Makka, hupitwa alfajiri ya siku ya Sikukuu. Basi wanahimizwa watu waombe Mungu sana hapo na wakumbuke neema kubwa hii aliyowapa Mwenyezi Mungu ya Uislamu.

**199.** Mwezi 9 wa mfunguo Tatu—tangu hizo zama za Nabii Ibrahim—wenye kuhiji huenda mahala mbali na hapo Makka panapoitwa Arafat (au Arafa), wakashinda hapo na wakakesha. Mwisho wake—katika zama za Ujahili—Maqureshi walijinata wakasema kuwa wao hawataondoka katika viunga vya Makka—vya Minaa na Muzdalifa na vinginevyo—wakenda Arafa. Basi walikuwa hawendi huko Arafa mwezi 9. Basi hapo wanalazimishwa Waislamu kuwa lazima wende huko Arafa mwezi 9 wakati wa Hija.

**200.** Mahaji hapo zama za Kijahili wanapokutana Minaa mwezi 11 na 12 na 13 huwa wanashindana kutaja matukufu ya wazee wao kwa mashairi na kwa namna nyinginezo. Ndiyo wanaambiwa hapa kuwa badili ya hivyo wawe wanamtaja Mwenyezi Mungu.

Na ilipoaemwa 'Na kuna baadhi . . .' ni kuonyesha kuwa tusishughulike kuomba dua za kutengenekewa na

(wanawake Waislamu) mpaka waamini. Na mtumwa mwenye kuamini ni bora kuliko muungwana mshirikina hata akikupendezeni. Hao (washirikina) wanaitia kwenye Moto. Na Mwenyezi Mungu anaitia kwenye Pepo na samahani, kwa amri Yake. Naye hueleza Aya Zake kwa watu ili wapate kukumbuka.

الْمُشْرِكِينَ حَتَّىٰ يُؤْمِنُوا ۚ وَلَعَبْدٌ مُؤْمِنٌ خَيْرٌ مِنْ
مُشْرِكٍ وَلَوْ أَعْجَبَكُمْ ۗ أُولَٰئِكَ يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ ۖ
وَاللَّهُ يَدْعُو إِلَى الْجَنَّةِ وَالْمَغْفِرَةِ بِإِذْنِهِ ۖ
وَيُبَيِّنُ آيَاتِهِ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ (٢٢١)

222. Na wanakuuliza juu ya hedhi; waambie huo ni uchafu. Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi (zao). Wala msiwakaribie mpaka watahirike. Wakishakutahirika basi waendeeni katika pale alipokuamrisheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na huwapenda wanaojitakasa.

وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الْمَحِيضِ ۖ قُلْ هُوَ أَذًى فَاعْتَزِلُوا
النِّسَاءَ فِي الْمَحِيضِ ۖ وَلَا تَقْرَبُوهُنَّ حَتَّىٰ
يَطْهُرْنَ ۖ فَإِذَا تَطَهَّرْنَ فَأْتُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ أَمَرَكُمُ
اللَّهُ ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ التَّوَّابِينَ وَيُحِبُّ الْمُتَطَهِّرِينَ (٢٢٢)

223. Wake zenu ni kama konde zenu. Basi ziendeeni konde zenu mpendavyo. Na tangulizieni (wema) nafsi zenu; na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba mtakutana naye (Mwenyezi Mungu). Na wapashe habari njema walioamini.

نِسَاؤُكُمْ حَرْثٌ لَكُمْ فَأْتُوا حَرْثَكُمْ أَنَّىٰ شِئْتُمْ ۖ
وَقَدِّمُوا لِأَنْفُسِكُمْ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ
مُلَاقُوهُ ۗ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ (٢٢٣)

224. Wala msifanye kuapa kwa jina la Mwenyezi Mungu ndiyo sababu ya kukuzuilieni na (kufanya mambo mazuri ya Uislamu), (kufanya mema) na kuogopa Mungu na kupatanisha baina ya watu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kujua.

وَلَا تَجْعَلُوا اللَّهَ عُرْضَةً لِأَيْمَانِكُمْ أَنْ تَبَرُّوا
وَتَتَّقُوا وَتُصْلِحُوا بَيْنَ النَّاسِ ۗ
وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ (٢٢٤)

225. Mwenyezi Mungu hatakushikeni kwa sababu ya kuapa kwenu kwa upuzi-upuzi. Bali atakushikeni kwa sababu (ya vile viapo) vilivyofanyiwa nguvu na nyoyo zenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mpole sana.

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلَٰكِنْ
يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا كَسَبَتْ قُلُوبُكُمْ ۗ
وَاللَّهُ غَفُورٌ حَلِيمٌ (٢٢٥)

226. Kwa wale wanaoapa kwamba watajitenga na wake zao, (muda wao) ni kungojewa miezi mine. Na kama wakirejea (wakatangamana na wake zao) basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

لِلَّذِينَ يُؤْلُونَ مِنْ نِسَائِهِمْ تَرَبُّصُ أَرْبَعَةِ
أَشْهُرٍ ۖ فَإِنْ فَاءُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ (٢٢٦)

---

ulimwengu tu—tuombe na dua za kutengenekewa na Akhera pia.

202. Na iliposemwa 'Kuwa sababu ya waliyoyachuma' ni kuonyesha kuwa dua hizo za kuomba kupata mema ya duniani na mema ya Kiyama ni Sharti — kwa kuyachuma (Kuyafanya) haya ya kukupa mema ya duniani na ya Akhera — si kwa kuomba tu basi. Jisaidie, na Mungu ndipo akusaidie.

203. Siku zinazohisabiwa ni zile siku 3—za mwezi 11 na baadaye — wanazokaa Minaa. Zimeitwa hivyo kwani huwa wanazihisabu tu siku kila wakati ili zimalizike warejee makwao — hamu ya kurejea makwao imewashika.

Basi wakaonewa huruma wakaambiwa kuwa wana khiari yao — wakitaka watatimiza siku 3 kukaa huko Minaa na wakitaka watakaa siku mbili tu.

204. Yaani huja wakaapa kwa Mtume kuwa wao ni watu wazuri, kumbe watu wabaya kabisa.

207. Watu wauzao nafsi zao . . . ni wanaotoa mali yao na wakazikalifu nafsi zao kufanya mambo anayoyataka Mwenyezi Mungu.

208. Wanalazimishwa Waislamu waitakidi amri zote za Uislamu—siyo hizi wanazikubali na hizi wanazikataa.

212. Wanaambiwa wasishughulikie dunia tu kama makafiri bali washughulikie yote mawili. Na Akhera ndiyo zaidi kwani ndiyo ya Milele.

227. Na wakiazimia kuwaacha (basi); Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kujua.

وَإِنْ عَزَمُوا الطَّلَاقَ فَإِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٢٧﴾

228. Na wanawake walioachwa wangoje (wasiolewe) mpaka tahara tatu zishe. Wala haiwajuzii kuficha (mimba) aliyoumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao, ikiwa wanamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho. Na waume wao wana haki ya kuwarejesha katika muda huo, kama wakitaka kufanya sulhu. Nao (wanawake) wanayo haki kwa Sharia (kufanyiwa na waume zao) kama ile haki iliyo juu yao kuwafanyia waume zao. Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.

وَالْمُطَلَّقَاتُ يَتَرَبَّصْنَ بِأَنفُسِهِنَّ ثَلَاثَةَ قُرُوءٍ ۚ
وَلَا يَحِلُّ لَهُنَّ أَن يَكْتُمْنَ مَا خَلَقَ اللَّهُ فِي
أَرْحَامِهِنَّ إِن كُنَّ يُؤْمِنَّ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ
وَبُعُولَتُهُنَّ أَحَقُّ بِرَدِّهِنَّ فِي ذَٰلِكَ إِنْ أَرَادُوا
إِصْلَاحًا ۚ وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۚ
وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٨﴾

229. Talaka (unazoweza kumrejea mwanamke) ni (zile zilizotolewa) mara mbili (za kwanza). Kisha ni kumweka kwa wema au kumwacha kwa ihsani. (Wala usiweze kumrejea tena mpaka aolewe na

الطَّلَاقُ مَرَّتَانِ ۖ فَإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٌ
بِإِحْسَانٍ ۗ وَلَا يَحِلُّ لَكُمْ أَن تَأْخُذُوا مِمَّا

---

214. Hapa Mwenyezi Mungu anabainisha — kama mahala pengi pengine katika Quran — kuwa lazima Mwislamu apate misukosuko katika kuuendesha Uislamu wake; hapana la faida lo lote linalopatikana kwa urakhisi. Na hii misukosuko ndiyo inayomtengeneza mtu kama tulivyotaja mbele katika Aya ya 153.

215. Waliuliza haya kabla hawajateremshiwa Hukumu za Mirathi. Ilipokuja hukumu ya Mirathi ilikatazwa kuwausia kitu hao wanaorithi kwani Mwenyezi Mungu kesha wawekea sehemu yao katika mali yako utakapokufa.

Ukitaka kuusia kitu wausie wasiokurithi; tena isiwe zaidi kuliko thuluthi ya mali yako.

Hao wanaokurithi unaweza kuwafanyia Wakfu siyo Wasia.

216. Aya hii waliyoifanya ni ya 217 waliifasiri vilivyo. Lakini katika Maelezo yao (mapotezo yao) wametia mstari wa maneno usiofahamika. Wameandika hivi, "au sivyo walikuwa wakichukia kupigana vita". Haijulikani wanasema nini. Muradi wao ni ule waliosema tukabainisha katika maelezo ya aya ya 195. Wamehizika.

217. Watu wa Mtume (Masahaba) walikabiliana na makafiri mwezi 30 Mfunguo tisa. Na wengine wakiona ni mwezi mosi wa Rajab siku hiyo. (Na mwezi wa Rajab hapana ruhusa ya kupigana). Basi Makureshi wakamchukulia Mtume kuwa kavunja hishima ya ile miezi mitukufu, na wakaja kumwuliza kuwa ndivyo hivyo? Mwenyezi Mungu akawajibu hivi.

219. Tumekwishataja kwenye maelezo ya Aya 106 ya hii *Suratil Baqarah* kuwa Ulevi na Kamari vilikuwa ni vitu vilivyowabobea Waarabu. Basi walipouliza hukumu yake waliharimishiwa kipande kipande. Mpaka mwisho wakaharimishiwa kabisa. Kwanza wakabainishiwa—katika Aya hii — madhara yake ya kiduniani. Tena ndio wakatajiwa madhara yake katika dini.

Na iliposemwa 'Vilivyokuzidieni' ni kuwahimiza watu watoe wasaidie wenziwao na wasaidie mambo mengine ya kheri.

Lakini wanaambiwa wasijitie taklifu kubwa, wao wala wasiwatie taklifu kubwa hizo wale walio chini yao wanaoendeshwa na wao. Wawatengezee hawa kwanza.

Wanaambiwa watoe Kinachozidi juu ya haya.

220. Ilipofanywa tashdidi juu ya kula, kwa dhuluma, mali ya mayatima, walezi wa mayatima (wengine) waliogopa sana. Wakaacha hata kula nao. Wakiwapikia chao mbali, kwa pesa zao (hao mayatima). Hawachanganyishi chao (walezi) na cha (hao mayatima) kwa kuogopa wasiwapunje katika kula.

Basi wakaambiwa kuwa si lazima kufikia daraja hiyo, na Mwenyezi Mungu anamjua nani anayefanya fisadi na nani anayefanya maslaha kwao (hao mayatima).

221. Aya hizi ni za kukataza kuozana baina ya makafiri (wasiokuwa Manasara na Mayahudi) na Waislamu—wanaume wa kwao hawaozwi wanawake wa kikwetu, na wanaume wa kikwetu hawaoi wanawake wa kikwao.

Ama Manasara na Mayahudi (ambao huitwa Ahlil Kitab—Wenye kupewa vitabu vya Mwenyezi Mungu) inawajuzia wanaume wetu (Waislamu) kuoa wanawake wa kikwao. Lakini wanawake wa kikwetu hawaolewi na wanaume wa kikwao. Haramu kabisa na haisihi ndoa hiyo.

آتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا إِلَّا أَن يَخَافَا أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ
اللَّهِ ۖ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ
فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا فِيمَا افْتَدَتْ بِهِ ۗ
تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا ۚ وَمَن يَتَعَدَّ
حُدُودَ اللَّهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٢٩﴾

mume mwengine maadam umetimiza mara tatu katika kumwacha ukimrejea). Wala si halali kwenu kuchukua cho chote mlichowapa (wake zenu), isipokuwa (wote wawili) wakiogopa ya kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu, hapo itakuwa hapana dhambi kwao (mwanamume wala mwanamke katika) kupokea (au kutoa) ajikomboleacho mwanamke. Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; basi msiiruke. Na watakaoiruka mipaka ya Mwenyezi Mungu, hao ndio madhalimu (wa nafsi zao).

فَإِن طَلَّقَهَا فَلَا تَحِلُّ لَهُ مِن بَعْدُ حَتَّىٰ تَنكِحَ
زَوْجًا غَيْرَهُ ۗ فَإِن طَلَّقَهَا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا
أَن يَتَرَاجَعَا إِن ظَنَّا أَن يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ ۗ وَتِلْكَ
حُدُودُ اللَّهِ يُبَيِّنُهَا لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٢٣٠﴾

230. Na kama amempa talaka (ya tatu) basi (mwanamke huyo) si halali kwake baada ya hapo mpaka aolewe na mume mwengine. Na (mwanamume huyo mwengine) akimwacha, basi hapo hapana dhambi kwao (mume yule wa kwanza na mwanamke huyo) kurejeana, wakiona watasimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na hii ni mipaka ya Mwenyezi Mungu anayoibainisha kwa watu wajuao (wanaotaka kujua).

وَإِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَبَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ
بِمَعْرُوفٍ أَوْ سَرِّحُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ ۚ وَلَا تُمْسِكُوهُنَّ
ضِرَارًا لِّتَعْتَدُوا ۚ وَمَن يَفْعَلْ ذَٰلِكَ فَقَدْ ظَلَمَ
نَفْسَهُ ۚ وَلَا تَتَّخِذُوا آيَاتِ اللَّهِ هُزُوًا ۚ وَاذْكُرُوا
نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَمَا أَنزَلَ عَلَيْكُم مِّنَ
الْكِتَابِ وَالْحِكْمَةِ يَعِظُكُم بِهِ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ
وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٣١﴾

231. Na mtakapowapa wanawake talaka, nao wakafikia kumaliza eda yao, basi warejeeni kwa wema au tokaneni nao kwa wema. Wala msiwaweke kwa kuwapa dhara mkaruka mipaka. Na atakayefanya hivyo, amejidhulumu mwenyewe. Wala msizifanyie mzaha Aya za Mwenyezi Mungu. Na mkumbuke neema za Mungu zilizo juu yenu, na (khasa ile neema ya) kuteremshiwa Quran na (kujuvywa) ilimu nyingine Anazokuonyeeni. Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

وَإِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَبَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَلَا
تَعْضُلُوهُنَّ أَن يَنكِحْنَ أَزْوَاجَهُنَّ إِذَا تَرَاضَوْا

232. Na mtakapowapa wanawake talaka, (ya kwanza au ya pili); nao wakamaliza eda yao, basi (nyinyi jamaa wa mke) msiwazuie kuolewa (au kurejewa) na waume zao endapo baina yao

223. Konde ni mahali palipoelekea kuwa mtu akipanda pataota. Na kwa mwanamke ni pale ambapo pataweza kuleta mtoto; si pale kinyume cha hapo.

224. Mtu akiapa kuwa hatafanya kitu fulani, kama vile kusema, "Wallahi! Sitasema na fulani." Basi asiwe akisema, "Mimi siwezi kusema naye kwani nimeapa kwa jina la Mungu"; asiseme hivyo. Bora aseme naye na atoe kafara.

225. Viapo vya mchezomchezo Mwenyezi Mungu havichukui.

226. Mwanamume akiapa kuwa hatamwingilia mkewe; basi mkewe atangoja muda wa mezi 4. Akitomwingilia atakwenda kumshitaki, na Kadhi atamlazimisha amwingilie au amwache. Haifai kabisa watu kutesana khasa baina ya mke na mume, na wengine anaochanganyika nao. Juu yao kustahamiliana.

227. Wamepachika — kidogo — la uwongo katika Aya walioifanya kuwa ni ya 228. Si kweli kipande hiki: "Na kama mke alikuwa hajalipwa mahari yake lazima kabla ya kutoa talaka ya mwisho." Hili tamko la "lazima"

بَيْنَهُمْ بِالْمَعْرُوفِ ۗ ذَٰلِكَ يُوعَظُ بِهِ مَنْ كَانَ
مِنْكُمْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ ذَٰلِكُمْ أَزْكَىٰ
لَكُمْ وَأَطْهَرُ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٣٢﴾

wamepatana kwa wema. Hayo anaonywa nayo yule miongoni mwenu anayemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Hayo ni mazuri mno kwenu na safi kabisa. Na Mwenyezi Mungu anajua, lakini nyinyi hamjui.

وَالْوَالِدَاتُ يُرْضِعْنَ أَوْلَادَهُنَّ حَوْلَيْنِ
كَامِلَيْنِ ۖ لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يُتِمَّ الرَّضَاعَةَ ۚ وَعَلَى
الْمَوْلُودِ لَهُ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۚ
لَا تُكَلَّفُ نَفْسٌ إِلَّا وُسْعَهَا ۚ لَا تُضَارَّ وَالِدَةٌ
بِوَلَدِهَا وَلَا مَوْلُودٌ لَهُ بِوَلَدِهِ ۚ وَعَلَى الْوَارِثِ
مِثْلُ ذَٰلِكَ ۗ فَإِنْ أَرَادَا فِصَالًا عَنْ تَرَاضٍ مِنْهُمَا
وَتَشَاوُرٍ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا ۗ وَإِنْ أَرَدْتُمْ أَنْ
تَسْتَرْضِعُوا أَوْلَادَكُمْ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِذَا سَلَّمْتُمْ
مَا آتَيْتُمْ بِالْمَعْرُوفِ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ
اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢٣٣﴾

233. Na wanawake waliozaa wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili, kwa anayetaka kukamilisha kunyonyesha; na ni juu ya baba (yake) chakula chao (hao watoto na mama) na nguo zao kwa Sharia. Wala haikalifishwi nafsi yo yote ila kwa kadiri ya wasaa wake. Mama asitiwe taabuni kwa ajili ya mtoto wake, wala baba (asitiwe taabuni) kwa ajili ya mtoto wake. Na juu ya mrithi (inapokuwa baba kafa) ni kama hivyo. Na kama wote wawili wakitaka kumwachisha ziwa (kabla ya miaka miwili), kwa kuridhiana na kushauriana, basi si kosa juu yao. Na kama mkitaka kuwapatia watoto wenu mama wa kuwanyonyesha (wengine wasiokuwa mama zao), basi haitakuwa dhambi juu yenu kama mkitoa (kuwapa hao wanyonyeshaji) mlichowaahidi kwa Sharia. na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anayaona yote mnayoyatenda.

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا
يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا ۖ
فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا
فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۗ وَاللَّهُ
بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٢٣٤﴾
وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا عَرَّضْتُمْ بِهِ مِنْ خِطْبَةِ

234. Na wale wanaofishwa (wanaokufa) miongoni mwenu na kuacha wake; hawa (wake) wangoje (wasiolewe) miezi mine na siku kumi. Na wanapofikia muda wao (wa kumaliza eda yao hiyo), basi si dhambi juu yenu kwa yale wanayoyafanyia nafsi zao (hao wanawake) kwa yanayowafiki (kufuata) Sharia. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za yote mnayoyatenda.

235. Wala si dhambi kwenu katika kupeleka habari ya posa kwa ishara tu (si kwa maneno)

---

halipo lakini ni jambo zuri kabisa kama lile la (1) na (2).

228. Mwanamke akiachwa hana ruhusa kuolewa na mume mwengine mpaka Eda yake ishe. Na Eda ni namna mbali mbali kwa wanawake namna mbali mbali.

(1) Akiachwa mwanamke mwenye mimba, basi Eda yake inakwisha kwa kuzaa. Pale pale akizaa anaweza kuolewa.

(2) Akiachwa mwanamke asiyeingia mezini kwa (a) kupindukia miaka au kwa (b) kutofika bado miaka ya kutoka hedhi au kwa (c) kuwa tabia yake (ndio maumbile yake) hatoki hedhi au kwa (d) sababu nyinginezo zilizomkata na hedhi; basi Eda yake ni mezi mitatu. Haolewi mpaka mezi 3 tangu siku aliyoachwa (sio tangu siku aliyoasiana na mumewe au aliyosafiri yeye au aliyoacha kukutana na mumewe—haya hayatazamwi). Inatazamwa siku ya kuachwa. Ikishatimia miezi 3 tangu siku aliyoachwa ataweza kuolewa.

(3) Na akiachwa mwanamke anayeingia mezini, basi Eda yake inakwisha kwa kumaliza Qur-i tatu. Na Qur-i ina khitilafu ya tafsiri. Kwa Kishafii ni Tahara tatu. Zikisha tahara 3 tangu kuachwa basi ataolewa. Na kwa Kiibadhi ni hedhi tatu. Zikisha hedhi tatu zilizokuja baada ya kuachwa ataolewa. Kuachwa, kufusahi na khuluu hukumu yake ni moja.

kuwaoa wake (walio edani), wala (hapana dhambi pia) katika kutia katika nyoyo zenu azma (za kuwaoa;) Mwenyezi Mungu anajua kwamba nyinyi mtawakumbuka. Lakini msifunge nao ahadi kwa siri (ya kuwaoa maadam eda haijesha); isipokuwa mseme maneno yaliyo mazuri. Wala msiazimie kufunga ndoa mpaka muda ulioandikwa (katika eda) ufike mwisho wake. Na jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo katika nafsi zenu, basi mwogopeni. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, (na) Mpole sana.

236. Si dhambi kwenu kama mkiwapa wanawake talaka ambao hamjawagusa au kuwabainishia mahari (yao). Lakini wapeni cha kuwaliwaza (kitoka nyumba); mwenye wasaa kadiri awezavyo, na mwenye dhiki kadiri awezavyo. Matumizi hayo (wanayopewa) yawe kama inavyosema Sharia. Ndio wajibu kwa wafanyao mema.

237. Na kama mkiwapa talaka kabla ya kuwagusa, na mmekwisha wawekea hayo mahari (makhsusi), basi (wapeni) nusu ya hayo mahari mliyoagana, isipokuwa wanawake wenyewe waache (ile nusu wasitake kitu), au yule (mume) ambaye kifungo cha ndoa ki mikononi mwake aache (haki yake ampe mahari kamili). Na kuachiana ndiyo kunakomkurubisha mtu sana na kumcha Mungu. Wala msisahau kufanyiana ihsani baina yenu; hakika Mwenyezi Mungu anayaona yote mnayoyafanya.

238. Angalieni sana Sala (zote kuzisali, khasa jamaa) na (khasa) ile Sala ya kati na kati. Na simameni kwa unyenyekevu katika kumwabudu Mwenyezi Mungu.

النِّسَاءِ أَوْ أَكْنَنتُمْ فِي أَنفُسِكُمْ ۚ عَلِمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ
سَتَذْكُرُونَهُنَّ وَلَٰكِن لَّا تُوَاعِدُوهُنَّ سِرًّا إِلَّا أَن
تَقُولُوا قَوْلًا مَّعْرُوفًا ۚ وَلَا تَعْزِمُوا عُقْدَةَ
النِّكَاحِ حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْكِتَابُ أَجَلَهُ ۚ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ
يَعْلَمُ مَا فِي أَنفُسِكُمْ فَاحْذَرُوهُ ۚ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ
غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿٢٣٥﴾

لَّا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِن طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ مَا لَمْ تَمَسُّوهُنَّ
أَوْ تَفْرِضُوا لَهُنَّ فَرِيضَةً ۚ وَمَتِّعُوهُنَّ عَلَى
الْمُوسِعِ قَدَرُهُ وَعَلَى الْمُقْتِرِ قَدَرُهُ مَتَاعًا بِالْمَعْرُوفِ ۖ
حَقًّا عَلَى الْمُحْسِنِينَ ﴿٢٣٦﴾

وَإِن طَلَّقْتُمُوهُنَّ مِن قَبْلِ أَن تَمَسُّوهُنَّ وَقَدْ
فَرَضْتُمْ لَهُنَّ فَرِيضَةً فَنِصْفُ مَا فَرَضْتُمْ
إِلَّا أَن يَعْفُونَ أَوْ يَعْفُوَ الَّذِي بِيَدِهِ
عُقْدَةُ النِّكَاحِ ۚ وَأَن تَعْفُوا أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ۚ
وَلَا تَنسَوُا الْفَضْلَ بَيْنَكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِمَا
تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢٣٧﴾

حَافِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَىٰ
وَقُومُوا لِلَّهِ قَانِتِينَ ﴿٢٣٨﴾

---

Basi maadam Eda haijesha hana ruhusa mwanamke kuolewa. Na akiolewa basi haisihi hiyo ndoa. Inakuwa wanazini tu muda wa kukaa kwao. Na watoto wanakuwa wana wa haramu.

Wanaambiwa hao walioachwa wasifiche kama wana mimba ili mtoto huyo ajulikane baba yake.

Na maadam Eda haikwisha (wala idadi za Talaka hazijesha pia), basi mume saa yo yote anaweza kumrejea huyo mke. Atashuhudisha mashahidi wawili na amjuvye huyo mke kuwa keshamrejea. Wala hana ruhusa huyo mke wala jamaa zake kukataa.

229. Na inakatazwa hapa (na katika Aya nyingine pia) kumtoza mwanamke fedha au kumsamehesha mahari wakati wa kumwacha. Dhulma mbaya mno na dhambi kubwa kabisa. Na watu siku hizi wanayafanya haya. Wanayaona mepesi kama maji ya kunywa, na hali ya kuwa mazito hayo mbele ya Mwenyezi Mungu.

Mahala pamoja tu ndipo inapokubaliwa mwanamke kutoa kikomboleo cha kujikomboa na ndoa. Wakati anapokuwa yule mwanamke hamtaki mume — pasina ubaya wo wote anaofanyiwa naye. Hamtaki tu na anaogopa kutotekeleza wajibu wake kwa mumewe. Basi atampa mahari yake, asalimike na wajibu huo ambao anaona hawezi kuutekeleza kwa kuwa hampendi tu huyo mume.

Na mume naye anaambiwa asifanye inda akakataa kumwacha. Naatake hicho alichotoa (ili akaolee mwengine), na amwache huyu akaolewe na anayemtaka. Hapana ruhusa kulipana mabaya.

230. Imeambiwa hapa kuwa uliyemwacha mara tatu huna ruhusa ya kumwoa mpaka aolewe na mume mwengine (ajue ulimwengu vipi ulivyo). Akiachwa huko ndipo unapopata ruhusa ya kumwoa; kwa kuwa sasa

239. Na kama mkiwa na khofu (kusali kidasturi; mmo katika kupigana; basi Salini) na hali ya kuwa mnakwenda kwa miguu au mmepanda (wanyama). Na mtakapokuwa katika amani, basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu (Salini) kama alivyokufunzeni yale mliyokuwa hamyajui.

فَإِنْ خِفْتُمْ فَرِجَالًا أَوْ رُكْبَانًا ۖ فَإِذَا أَمِنتُمْ
فَاذْكُرُوا اللَّهَ كَمَا عَلَّمَكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ ﴿٢٣٩﴾

240. Na wale wanaofishwa (wanaokufa) miongoni mwenu na wakawacha wake, wawausie (mawarithi wao) kwa ajili ya wake zao kupata matumizi kwa mwaka mmoja bila ya kutolewa (katika majumba waliyokuwamo, ya waume zao). Na kama wanawake (wenyewe) wakiondoka, basi si kosa juu yenu kwa yale waliyoyafanya kwa nafsi zao wenyewe yanayofuata Sharia. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا
وَصِيَّةً لِّأَزْوَاجِهِم مَّتَاعًا إِلَى الْحَوْلِ غَيْرَ
إِخْرَاجٍ ۚ فَإِنْ خَرَجْنَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا
فَعَلْنَ فِي أَنفُسِهِنَّ مِن مَّعْرُوفٍ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ
حَكِيمٌ ﴿٢٤٠﴾

241. Na wanawake walioachwa wapewe cha kuwaliwaza (kitoka nyumba) kwa namna nzuri inayosema Sharia. Huu ni wajibu kwa wamchao Mwenyezi Mungu.

وَلِلْمُطَلَّقَاتِ مَتَاعٌ بِالْمَعْرُوفِ ۖ حَقًّا
عَلَى الْمُتَّقِينَ ﴿٢٤١﴾

242. Namna hivi anakubainishieni Mwenyezi Mungu Aya zake ili mpate kufahamu.

كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٢٤٢﴾

243. Hukusikia (habari za) wale waliotoka katika majumba yao (wanawakimbia maadui zao), nao walikuwa maelfu-elfu wakiogopa mauti? Mwenyezi Mungu akawaambia: "Kufeni." (Wakafa bure bila

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ خَرَجُوا مِن دِيَارِهِمْ وَهُمْ
أُلُوفٌ حَذَرَ الْمَوْتِ فَقَالَ لَهُمُ اللَّهُ مُوتُوا

---

kesha ujua ulimwengu kidogo, basi inatarajiwa mtaishi kwa vizuri mkhatimishane kwa kheri.

Lakini wasiojua hikima za Mwenyezi Mungu zilizomo katika Shāria yake huona muradi ni kuolewa tu japo dakika moja. Basi huagana na watu (wanaoitwa Muhalili) kuwaolea wake zao na kuwaingilia dakika moja hiyo; kisha wawaache wawaoe wenyewe.

Hapana ruhusa hayo katika Sharia. Mwenyezi Mungu amewalani wanaofanya haya. Kasema haya Mtume kwa hadithi iliyotajwa na maimamu hawa: Ahmad Bin Hambal, Abu Daud, Attirmidhy, Annassai na wengineo.

231. Wanahimizwa waume wawarejee wake zao upesi kabla eda haijesha wasije wakaolewa na waume wengine wakajuta — zimwi likujualo halikuli likakwisha.

Lakini wanaambiwa wawarejee kwa nia njema; sio kuja kuzidi kuwadhili kama walivyowadhili mara ya kwanza.

232. Mkiwazuilia kurejeana na waume wao—nao wanapendana—watazini nao badili ya kuoana iwe 'Wamevunja Nyumba Wamejenga Upenu.' Asiyefuata anayoyasema Mwenyezi Mungu na Mtumewe ataharibikiwa duniani na Akhera.

233. Sana mtoto hunyonyeshwa na mama yake muda wa miaka miwili. Na anaweza kuendelea kumnyonyesha hata baada ya miaka miwili. Si haramu. Lakini si vizuri. Na anaweza huyo mama mtu—akiwafikiana na baba mtu—kumwachisha kabla ya miaka miwili maadam wanaona kuwa hatadhurika huyo mtoto.

Na baba akiwa kamwacha yule mama—na mama anaendelea kumnyonyesha yule mtoto—basi itampasa huyo baba kumpa ijara yake huyo mama ya kuweza kupatia humo chakula chake huyo (mama) na nguo zake na maskani yake na gharama zake nyinginezo. Asiambiwe 'Mtoto wako mwenyewe huyo! Utamfanyia bure hayo!' Atampata wapi basi huyo mwanamke mtu wa kumlisha na kumvika, naye kawachwa na huyo baba wa mtoto wala hana mume mwengine. Ndiyo maana ikawa juu ya huyo baba gharama zake.

Na huyo mama naye inataka asimfanyie tashdidi nyingi huyo baba kwani—kila namna—huyo mtoto ni wao wote; atakuja kuwafaa wote wawili Inshallah.

Na ikiwa hana baba—wala hana mali—basi wale jamaa zake sana (huyo mtoto) wa kuweza kurithiana ndio watakaotoa gharama hizo kumpa mama.

Na wakiwafikiana kuwa anyonyeshwe na mtu mwengine — asinyonyeshwe na mama yake — basi. Lakini kwa sharti isiwe anadhuriwa huyo mtoto anayenyonyeshwa, wala huyo mama yake.

sababu yo yote); kisha akawahuisha (ili awaonyeshe kuwa kufa hakukushikamana na kupigana tu). Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhili juu ya watu, lakini watu wengi hawashukuru.

244. Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anasikia na anajua (kila kitu).

245. Ni nani atakayemkatia Mwenyezi Mungu sehemu bora (ya mali yake kwa kuwapa masikini na kwa kutoa katika mambo mengine ya kheri) ili Mwenyezi Mungu amzidishie mzidisho mwingi, na Mwenyezi Mungu ndiye anayezuia na ndiye anayetoa, na Kwake (nyote) mtarejeshwa.

246. Hukusikia habari ya wakubwa wa Kibanii Israili baada ya Musa, walipomwambia Nabii wao: "Tuwekee mfalme ili tupigane katika njia ya Mwenyezi Mungu." Yeye (Mtume wao) akasema: "Haielekei ya kuwa hamtapigana ikiwa mtaandikiwa kupigana?" Wakasema: "Itakuwaje tusipigane katika njia ya Mwenyezi Mungu, na hali tumetolewa katika majumba yetu na watoto wetu?" Lakini walipoandikiwa kupigana waligeuka, isipokuwa wachache miongoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anawajua sana madhalimu.

247. Na huyo Mtume wao akawaambia: "Mwenyezi Mungu amekuchagulieni Taluti kuwa mfalme." Wakasema: "Vipi atakuwa na ufalme juu yetu, na hali sisi tumestahiki zaidi kupata ufalme kuliko yeye, naye hakupewa wasaa wa mali?" Akasema: 'Mwenyezi Mungu amemchagua juu yenu na amemzidishia wasaa wa ilimu na kiwiliwili. Na Mwenyezi Mungu humpa ufalme Wake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa (na) Mwenye kujua.'

ثُمَّ أَحْيَاهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ
وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٢٤٣﴾

وَقَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ
سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٤﴾

مَّن ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضَاعِفَهُ
لَهُ أَضْعَافًا كَثِيرَةً ۚ وَاللَّهُ يَقْبِضُ وَيَبْسُطُ
وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٤٥﴾

أَلَمْ تَرَ إِلَى الْمَلَإِ مِن بَنِي إِسْرَائِيلَ مِن بَعْدِ
مُوسَىٰ إِذْ قَالُوا لِنَبِيٍّ لَّهُمُ ابْعَثْ لَنَا مَلِكًا
نُّقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۖ قَالَ هَلْ عَسَيْتُمْ إِن
كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ أَلَّا تُقَاتِلُوا ۖ قَالُوا وَمَا لَنَا
أَلَّا نُقَاتِلَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَدْ أُخْرِجْنَا مِن دِيَارِنَا
وَأَبْنَائِنَا ۖ فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقِتَالُ تَوَلَّوْا
إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٢٤٦﴾
وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ اللَّهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَالُوتَ
مَلِكًا ۚ قَالُوا أَنَّىٰ يَكُونُ لَهُ الْمُلْكُ عَلَيْنَا وَنَحْنُ
أَحَقُّ بِالْمُلْكِ مِنْهُ وَلَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِّنَ الْمَالِ ۚ
قَالَ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَاهُ عَلَيْكُمْ وَزَادَهُ بَسْطَةً
فِي الْعِلْمِ وَالْجِسْمِ ۖ وَاللَّهُ يُؤْتِي مُلْكَهُ مَن
يَشَاءُ ۚ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٧﴾

---

236. Mambo ya kuachana yanakatazwa kweli kweli. Na yakitokea basi lazima afanyiwe ihsani kubwa yule anayewachwa. Kama kufanyiwa haya:-

(a) Kupewa mahari yaliyosalia; (b) Kupewa pesa nyingine za 'Kitoka Nyumba'; (c) Kupewa nguo na makazi na chakula cha kila siku kama dasturi mpaka eda yake ishe; japo ikichukua muda mrefu; (d) Kuachiwa achukue vitu vyake mwenyewe na ulivyompa wewe kwa huba yenu. Hapana ruhusa kumnyang'anya cho chote.

Na yako mengine pia, tutayataja Inshallah katika *Suratut Talaq.*

237. Ukimuoa mwanamke ukamwacha kabla ya kuingia nyumbani (kumwingilia), utampa nusu ya mahari yaliyotajwa. Na kama umekwishampa atakurejeshea nusu yake.

Lakini bora zaidi kwa mume ikiwa hakumpa bado ampe yote. Na ikiwa amekwisha kumpa asitake kurejeshewa. Na vizuri vile vile kwa mwanamke kurejesha zote kama keshapewa na kuzikataa zote kama hajapewa. Kila mmoja afanye moyo mkubwa juu ya pesa, asiwe na pupa la kupata tu.

Na kama ilikuwa hayakutajwa mahari kiasi gani wala hawakuagana kwa kiasi gani, basi ampe kitu tu cho chote kiasi cha kumliwaza. Na haya ndiyo yaliyotajwa katika Aya ya 236.

Na imehimizwa sana watu wasiwache kufanyiana ihsani; wasisahau ihsani walizofanyiwa.

238. Imehimizwa Sala zote kuzisali jamaa khasa hiyo ya Kati na Kati. Wengine wamesema kwamba Sala ya

248. Na Nabii wao akawaambia: "Alama ya ufalme wake ni kukujieni lile sanduku ambalo mna ndani yake kituliza nyoyo zenu, kitokacho kwa Mola wenu, na mna masazo ya yale waliyoyaacha watu wa Musa na watu wa Harun; wakilichukua Malaika (kukuleteeni yaani limo katika hifadhi yao japo limechukuliwa juu ya gari). Bila shaka katika hayo mna dalili kwenu (ya ufalme wake juu yenu) ikiwa nyinyi mnaamini."

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ آيَةَ مُلْكِهِ أَنْ
يَأْتِيَكُمُ التَّابُوتُ فِيهِ سَكِينَةٌ مِنْ رَبِّكُمْ
وَبَقِيَّةٌ مِمَّا تَرَكَ آلُ مُوسَىٰ وَآلُ هَارُونَ تَحْمِلُهُ
الْمَلَائِكَةُ ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ
مُؤْمِنِينَ ﴿٢٤٨﴾

249. Basi Taluti alipoondoka na majeshi, alisema: "Mwenyezi Mungu atakufanyieni mtihani kwa mto (mtakaokutana nao njiani huko mnakokwenda). Basi atakayekunywa humo si pamoja nami, na asiyekunywa atakuwa pamoja nami; ila atakayeteka kwa kiasi cha kujaza kitanga cha mkono wake (akanywa hayo tu, huyo hana makosa)." Lakini walikunywa humo isipokuwa wachache tu miongoni mwao. Basi alipouvuka yeye na (wakauvuka) wale walioamini pamoja naye, walisema: "Leo hatumwezi Jaluti na majeshi yake." Wakasema wale wenye yakini ya kukutana na Mola wao: "Makundi mangapi madogo yameshinda makundi makubwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wafanyao subira."

فَلَمَّا فَصَلَ طَالُوتُ بِالْجُنُودِ قَالَ إِنَّ
اللَّهَ مُبْتَلِيكُمْ بِنَهَرٍ فَمَنْ شَرِبَ مِنْهُ
فَلَيْسَ مِنِّي وَمَنْ لَمْ يَطْعَمْهُ فَإِنَّهُ مِنِّي
إِلَّا مَنِ اغْتَرَفَ غُرْفَةً بِيَدِهِ ۚ فَشَرِبُوا مِنْهُ
إِلَّا قَلِيلًا مِنْهُمْ ۚ فَلَمَّا جَاوَزَهُ هُوَ وَالَّذِينَ آمَنُوا
مَعَهُ قَالُوا لَا طَاقَةَ لَنَا الْيَوْمَ بِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ ۚ
قَالَ الَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُمْ مُلَاقُو اللَّهِ كَمْ مِنْ
فِئَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيرَةً بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ
وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٢٤٩﴾

---

Kati na Kati ni Sala ya Adhuhuri—inasaliwa kati ya mchana wakati wa jua kali kabisa khasa kama katika nchi za Bara Arabu. Watu huona taabu kwenda kuisali misikitini jamaa. Basi ndio wakahimizwa hivi.

Na wengine wanasema kwamba Sala ya Kati na Kati ni Sala ya Alfajiri inayosaliwa wakati wa Kati na Kati — si wa mchana wala si wa usiku. Na wakati ambao ndipo usingizi unaposhtadi. Basi wakahimizwa kuacha huo usingizi na kwenda misikitini kusali jamaa.

Na inahimizwa wanaposali watu wasali kwa unyenyekevu—wajue kuwa wamesimama mbele ya Mwenyezi Mungu wakati huo.

Wamepachika neno lao wenyewe tu katika hii Aya walioifanya kuwa ni ya 239. Hili la kusema: "Lakini kwa hakika Sala ya katikati ile kila Sala inayomkuta mtu katikati ya shughuli zake." Sivyo hivi ilivyopokewa kwa Mtume wala Masahaba wala wanavyuoni wa kutegemewa.

240. Aya hii sasa—baada ya kuja hukumu za mirathi na ikawa wanawake wanapata robo au thumni ya mali ya waume zao—si lazima kutumika *(Mansukh)*.

Zamani hapo ilikuwa ni wajibu wa kila mume akijiona anakufa amwandikie mkewe kitu cha kumtosha mwaka mzima, kwa maskani yake na kula kwake na kuvaa kwake mpaka mwaka wishe. Na kama hajawahi kuusia watalazimishwa wale jamaa zake mume wamfanyie haya. Wala wasimtoe hapo nyumbani; ila akitaka mwenyewe kutoka, basi.

Ilipokuja hukumu ya mirathi imeambiwa apewe robo ya mali ya mume (ikiwa hana watoto), na apewe thumni (inapokuwa ana watoto huyo mume), na akae eda muda wa mezi 4 tu na siku 10. Ukisha muda huu anaweza kuolewa.

241. Unapomwacha mwanamke inataka umpe kitu juu ya yale mahari anayokudai. Na watu wa pande zetu hizi hufanya kinyume cha hayo—huwatoza wanawake fedha! Dhulma iliyoje hii!

243. Aya hii ni ya kuwahimiza watu kupigania dini ya Mwenyezi Mungu na kuwatoa woga kuwa kufa hakukukhusika na kupigana. Saa ikishafika basi; utakufa juu ya kiti chako unazungumza!

Katika Aya ya 56 ya hii *Al Baqarah* tumerejeza uwongo wa kukanusha kwao kufufuliwa hapa duniani baadhi ya waliokufa — kwa kuonyesha Mwenyezi Mungu kudra yake.

250. Na walipotoka kupambana na Jaluti (mfalme wa hao maadui) na majeshi yake, walisema hao watu wa Taluti: "Mola wetu! Tumiminie subira, na uithibitishe miguu yetu, na utusaidie juu ya watu hawa makafiri."

وَلَمَّا بَرَزُوا لِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ قَالُوا رَبَّنَا أَفْرِغْ
عَلَيْنَا صَبْرًا وَثَبِّتْ أَقْدَامَنَا وَانْصُرْنَا عَلَى
الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٥٠﴾

251. Basi (hao watu wa Taluti) wakawaendesha mbio (hao maadui zao) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu; na Daudi akamwua Jaluti, na Mwenyezi Mungu akampa (huyu Daudi) ufalme na hikima (Utume) na akamfundisha aliyoyapenda. Na kama Mwenyezi Mungu asingalizuia watu, baadhi yao kwa wengine, kwa yakini ardhi ingaliharibika. Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila (kubwa) juu ya walimwengu wote.

فَهَزَمُوهُمْ بِإِذْنِ اللَّهِ وَقَتَلَ دَاوُودُ جَالُوتَ
وَآتَاهُ اللَّهُ الْمُلْكَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَهُ
مِمَّا يَشَاءُ ۗ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ
بِبَعْضٍ لَفَسَدَتِ الْأَرْضُ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ
ذُو فَضْلٍ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٢٥١﴾

252. Hizi ni Aya za Mwenyezi Mungu, tunakusomea kwa haki. Na bila shaka wewe ni miongoni mwa (hao) Mitume (aliowaleta Mwenyezi Mungu).

تِلْكَ آيَاتُ اللَّهِ نَتْلُوهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ ۚ
وَإِنَّكَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٢٥٢﴾

253. Mitume hao tumewafadhilisha baadhi yao zaidi kuliko wengine. Miongoni mwao wako ambao Mwenyezi Mungu alisema nao; na wengine akawapandisha katika vyeo vikubwa kabisa. Na Isa Mwana wa Mariyamu tukampa hoja zilizo wazi, na tukamtia nguvu kwa Roho Takatifu. Na kama Mwenyezi Mungu angalitaka wasingalipigana wale waliokuwa baada yao (baada ya hao Mitume) baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi. Lakini walihitalifiana. Kwa hivyo wako miongoni mwao walioamini, na wengine miongoni mwao waliokufuru. Na kama Mwenyezi Mungu angalipenda wasingalipigana; lakini Mwenyezi Mungu hufanya anayoyataka.

تِلْكَ الرُّسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ
بَعْضٍ ۘ مِنْهُمْ مَنْ كَلَّمَ اللَّهُ ۖ وَرَفَعَ بَعْضَهُمْ
دَرَجَاتٍ ۚ وَآتَيْنَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ الْبَيِّنَاتِ
وَأَيَّدْنَاهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ ۗ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا اقْتَتَلَ
الَّذِينَ مِنْ بَعْدِهِمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمُ
الْبَيِّنَاتُ وَلَٰكِنِ اخْتَلَفُوا فَمِنْهُمْ مَنْ آمَنَ وَمِنْهُمْ
مَنْ كَفَرَ ۚ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا اقْتَتَلُوا وَلَٰكِنَّ اللَّهَ
يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ ﴿٢٥٣﴾

---

245. Hapa watu wanahimizwa kutoa katika njia za kheri. Na kuwa hata ukitoa kidogo Mungu atakupa kikubwa huko Akhera na akutilie baraka hapa.

247. Hapa Mwenyezi Mungu anatia nguvu habari ya Ilimu na Siha. Mwenye Ilimu na Siha ndiye anayestahiki kupewa ukubwa wa kuendesha watu na mambo yao. Na ilimu haikamiliki katika kiwiliwili chenye siha mbovu. Uislamu unahimiza sana—katika Quran na Hadithi—juu ya kutafuta ilimu na kurai (kuchunga) siha.

Wamepotoa mahala pawili katika hii Aya waliyosema kuwa ni Aya ya 248. Kwanza kusema kwao kuwa:

(a) Talut "mfalme mmoja wa Kiisraeli, aliyekuwako miaka mia mbili kabla ya Nabii Daud". Mwenyezi Mungu kasema hapa kuwa katika vita hivi alivyopiganisha Mfalme Talut alipigana kwa ushujaa mkubwa, mtu aliyekuwa akiitwa Daud, akamwua Jalut (mfalme wa maadui) na akapewa yeye ufalme, kisha akapata na Utume. Wao wanajifanya wanajua kuliko Mwenyewe Mwenyezi Mungu. Wanasema kuwa Talut alikuwa miaka mia mbili kabla ya kuzaliwa Nabii Daud.

(b) Tabuti (na wameliharibu vile vile katika 249) Wakasema kuwa Tabuti maana yake Moyo. Wamepindua hivi, na hali ya kuwa wanajua kuwa Tabuti maana yake Sanduku, kama walivyofasiri wafasiri wa Qurani wote, na wafasiri wa maneno magumu ya Qurani wote, na wenye kufasiri maneno ya Kiarabu yo yote. Wote wamesema kuwa Tabuti maana yake Sanduku. Na Mwenyezi Mungu ndivyo alivyosema hapa kuwa "Atakuleteeni lile Sanduku (lenu) ambalo mna ndani yake kituliza nyoyo zenu, kitokacho kwa Mola wenu, na mna masazo ya yale waliyoyaacha watu wa Musa na watu wa Harun." Hilo ni Sanduku ambalo ndani yake zilikuwamo hizo mbao ambazo ndani yake zimeandikwa zile amri kumi alizoteremshiwa Nabii Musa, na yalikuwamo ndani yake masazo